# ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005 - 2010

# UTANGULIZI

## HALI ILIVYO DUNIANI NA MAJUKUMU YALIYO MBELE YETU

### Hali Ilivyo Duniani

1. Dunia ya leo imegawanyika katika maeneo mawili makubwa. Kuna dunia ya nchi za Kaskazini ambazo zimeendelea, na dunia ya nchi za Kusini zilizo nyuma. Nchi za Kaskazini zimeendelea kwa vile zimekamilisha kwa sehemu kubwa mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi na pia mapinduzi ya viwanda na sasa ziko katika mapinduzi ya teknolojia ya habari. Kutokana na matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia katika uzalishaji mali na utoaji huduma, uchumi wa nchi hizi za Kaskazini una tija kubwa na hivyo huzalisha ziada nyingi. Nguvu kubwa inayousukuma uchumi wa nchi hizi ni ushindani katika mazingira ya uchumi wa soko. Maendeleo ya kiuchumi yameibua maendeleo makubwa ya kijamii na hivyo umaskini, ujinga na maradhi kutokomezwa kwa kiasi kikubwa.

2. Nchi za Kusini zina udhaifu wa aina mbili. Kwanza ni nchi zilizo nyuma kiuchumi, yaani nchi zisizotumia sayansi na teknolojia bora katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma na hivyo uchumi wake una tija ndogo na unaishia kutoa ziada ndogo. Nchi hizi hazijalikabili suala la msingi la mapinduzi ya kilimo wala la mapinduzi ya viwanda. Udhaifu wa pili ni kuwa nchi za Kusini kwa ujumla ni nchi tegemezi. Mahitaji yao ya sekta ya kisasa pamoja na sehemu kubwa ya mahitaji ya nyumbani na binafsi yanaagizwa kutoka nchi za Kaskazini na mazao yao hayasindikwi au kutengenezwa nchini mwao, bali karibu yote huuzwa nje yakiwa ghafi. Kwa nchi nyingi za Kusini, hasa za Afrika, hata bajeti za Serikali zinategemea ruzuku kutoka kwa wahisani wa nchi za Kaskazini.

**Utandawazi Hauepukiki**

3. Pamoja na tofauti kubwa iliyopo kati ya uchumi wa kisasa wa nchi za Kaskazini na uchumi ulio nyuma na tegemezi wa nchi za Kusini**, uchumi wa dunia ni mmoja unaotawaliwa na nguvu na kanuni zile zile.** Uchumi wa soko maana yake ni uhuru wa mitaji, bidhaa, wataalamu, sayansi, teknolojia na habari kuzagaa kokote duniani zikitafuta maslahi yenye tija na faida bila kukwazwa na mipaka ya nchi wala kanda. Huo ndio utandawazi. **Utandawazi si suala la hiari ya nchi au ya viongozi wa nchi. Utandawazi ni suala la hali halisi.** Ni suala la uwazi na ukweli. Hali ya utandawazi inafanana na hali inayotawala uhusiano kati ya mito na bahari. Mali na utajiri nao hutiririka kutoka nchi za Kusini kwenda nchi za Kaskazini kutokana na nguvu za soko. Huu ndio ukweli wa utandawazi.

4. Kutokana na hali hii, ni jambo la ukweli mtupu kwamba nchi za Kaskazini zina nafasi kubwa sana ya kushiriki katika uchumi wa ushindani wa dunia ya utandawazi. Nchi hizo ndizo zenye bidhaa maridhawa ambazo ni pamoja na mashine na mitambo, mitaji, wataalamu na teknolojia. Ili nchi za Kusini ziweze kushiriki (kuwa wabia) katika uchumi huu wa soko na wa ushindani, lazima nchi moja moja na kwa kushirikiana na nchi nyingine kikanda, kujijengea uwezo na mikakati ya kuzalisha, kusindika na kutengeneza bidhaa bora na nyingi na kuzipenyeza kwenye masoko ya kimataifa kutokana na kujijengea msingi wa uchumi wa kisasa ili kushiriki huko katika soko la kimataifa kuwe endelevu. Hali halisi hii inaonyesha ilivyo vigumu kwa nchi za Kusini kujikwamua kwenye hali ya uchumi ulio nyuma na tegemezi ili kuingia kwenye mkondo wa uchumi wa kisasa.

5. Hata hivyo, mfumo wa uchumi wa dunia wa leo wa ushindani wa soko na utandawazi , pamoja na ukatili wake una sura ya hisani pia. Nchi za Kusini ambazo uongozi wake umeonyesha **ushupavu, umakini, umahiri na uadilifu** katika kuyakabili matatizo ya maendeleo ya nchi zao, zimeweza kupata fursa za aina kadhaa katika nyanja za kimataifa zinazozifungulia milango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hisani hii ya nchi za Kaskazini si kielelezo cha

wema wa matajiri hao. Zaidi ni matokeo ya kampeni ambazo zimeendeshwa kwa miaka mingi sasa na viongozi mashuhuri wa nchi za Kusini za kuukosoa **mfumo kandamizi wa kinyonyaji na usio wa hak**i wa uchumi wa dunia. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere na sasa Rais Benjamin W. Mkapa ni miongoni mwa walioongoza harakati hizo. Kwa bahati nzuri, kampeni hizi dhidi ya mfumo usio wa haki wa uchumi wa dunia zinaungwa mkono katika nchi za Kaskazini na baadhi ya watu mashuhuri, taasisi na jumuiya za raia wa nchi hizo.

6. Kuna mifano michache ya fursa zilizoweza kupatikana katika nchi za Kusini kutoka nyanja za kimataifa kutokana na madai na kosoa za wana harakati wa mfumo mpya wa uchumi duniani, kwa mfano:-

(a) Nchi za Kaskazini zimeweza kutoa fursa maalumu kwa nchi za Kusini kuuza bidhaa na mazao katika masoko yao k.m. EBA, AGOA. n.k. Tatizo kwa nchi za Kusini kama Tanzania ni kutokuwa na mazao na bidhaa nyingi na zenye ubora za kuuza kwenye masoko hayo.

(b) Wenye mitaji katika nchi za Kaskazini wanajitokeza kuwekeza katika nchi za Kusini pale ambapo mazingira yanavutia. Kutokana na mazingira muafaka ambayo ni pamoja na sheria zenye masharti yanayovutia na hali ya amani na utulivu nchini, Tanzania sasa ni miongoni mwa nchi zinazoongoza katika Afrika kwa kuvutia wawekezaji.

( c) Mashirika ya kimataifa na nchi wahisani zinachangia maendeleo ya barabara za kisasa na miundombinu mingine katika nchi za Kusini kwa msingi wa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu. Fursa hizi zinasaidia kusukuma maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi zinazohusika. Tanzania imefaidika na fursa za mikopo ya aina hii.

(d) Mashirika ya kimataifa na nchi za Kaskazini zimebuni mpango wa kuzifutia madeni nchi maskini sana, na

Tanzania imefaidika na mpango huo. Suala la nchi maskini kufutiwa madeni limepata msukumo mpya na mkubwa kutokana na nchi nane tajiri (G8) za Kaskazini kukubali mapendekezo ya Tume ya Afrika ya Tony Blair, ambayo Rais Benjamin W. Mkapa alikuwa mjumbe.

(e) Benki ya Dunia imetoa kwa Tanzania mkopo wa mabilioni ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na mkopo mwingine mkubwa kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Mikopo hii ya Benki ya Dunia ikichanganywa na mchango wa Serikali yetu na nguvu za wananchi wenyewe ni msingi mkubwa wa mapinduzi ya elimu katika nchi yetu.

(f) Aidha, wahisani kutoka nchi za Kaskazini wanatoa misaada mikubwa na mingi kuzisaidia nchi za Kusini kukabiliana na majanga ya maradhi hasa ukimwi, kifua kikuu na malaria; na kutoa chanjo mbalimbali kwa mama wajawazito na watoto.

7. Uchambuzi katika Utangulizi huu umekusudiwa kuonyesha wazi wazi kuwa mfumo wa uchumi wa soko wa dunia, na utandawazi unatoa nafasi ndogo sana kwa nchi za Kusini kufanya mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kijamii ya nchi zao. Hata hivyo, nchi za Kusini zenye **uongozi shupavu, makini, mahiri na adilifu** zinaweza kuzivusha nchi zao kufikia maendeleo endelevu ili mradi wazijue njia za kuzitumia fursa hizi zinazotolewa na jumuiya ya kimafaifa. Wananchi wakichagua tena Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005, kitahakikisha kuwa Serikali zinaendeleza na kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa uliokwisha jengwa ili fursa za kiuchumi na kijamii zinazoweza kupatikana na zinazotolewa nayo ziendelee kuchangia katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu wetu.

## Majukumu Yaliyo Mbele Yetu

8. CCM inapenda kutamka bayana majukumu mawili ya msingi. **Jukumu la kwanza ni kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea**. jukumu hilo ni letu Watanzania**.** Wahisani wanatuunga mkono tu. **Jukumu la pili ni kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umasikini.**

9. Umasikini unaowasibu wananchi wetu na mamilioni ya watu katika nchi za Kusini ni matokeo ya uchumi ulio nyuma na tegemezi. Njia pekee ya kuondokana na uchumi huu unaozaa unyonge na shida katika jamii ni kujenga msingi wa uchumi wa kisasa ili kukuza uchumi na kuutokomeza umasikini hatua kwa hatua. Ilani hii ni kielelezo cha dhamira ya CCM ya kuiendeleza kazi nzuri iliyokwisha kufanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya Rais Mkapa. Ikichaguliwa tena, CCM itahahikikisha kwamba Serikali ya Awamu ya Nne inaiendeleza kazi ya kukuza uchumi na kupambana na umasikini kwa **"ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya."**

# SURA YA KWANZA

## MAFANIKIO YA KIUCHUMI NA KIJAMII YA MIAKA 10 YA SERIKALI YA AWAMU YA TATU

10. Hali ya uchumi na huduma za jamii haikuwa ya kuridhisha wakati Rais Benjamin W. Mkapa alipoingia madarakani mwaka 1995. Ukuaji wa uchumi ulikuwa 3.6%, mfumuko wa bei ulikuwa juu kwa kiwango cha asilimia 27; mapato ya Serikali yalikuwa ya wastani wa shilingi 25 bilioni kwa mwezi; uhusiano wa Tanzania na wahisani wa nje ulikuwa umeathirika vibaya; hali ya elimu na afya haikuwa ya kutia matumaini; na miundombinu ya kiuchumi na kijamii ilihitaji ukarabati na matengenezo makubwa.

11. Miaka kumi (1995-2005) ya Awamu ya Tatu ya Serikali ya CCM imeshuhudia kazi kubwa ya kurekebisha uchumi, kupitisha sheria za kuimarisha usimamizi na nidhamu katika ukusanyaji na matumizi ya fedha za Serikali, kuziba mianya ya rushwa na kuunda na kuimarisha vyombo vya kupambana na rushwa. Kutokana na kazi hii kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali chini ya uongozi shupavu wa Rais Mkapa hali ya uchumi imeanza kuimarika na kuwapa wananchi matumaini na huduma za jamii zimeanza kuridhisha.

12. Katika kipindi hiki cha Awamu ya Tatu ukuaji wa uchumi umefikia asilimia 6.7; mfumuko wa bei umeshuka kutoka asilimia 27 mwaka 1995 hadi asilimia 4.5 mwaka 2005 mwanzoni; mapato ya Serikali yameongezeka kutoka wastani wa shilingi 25 bilioni kwa mwezi mwaka 1995 hadi shilingi 160 bilioni kwa mwezi katika nusu ya kwanza 2005; miundombinu ya barabara za lami na madaraja ya kisasa yamejengwa katika kipindi hiki kuliko katika kipindi kingine chochote katika historia ya nchi yetu; upanuzi wa vyombo vya habari na mawasiliano ya simu za mkononi yameiweka Tanzania katika nafasi ya kupigiwa mfano katika Afrika.

13. Kutokana na mafanikio ya kiuchumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu, na umahiri wa uongozi wa Taifa wa kujenga uhusiano mwema

na nchi na mashirika ya kimataifa, nchi yetu imeweza kufanya mapinduzi makubwa katika sekta za elimu, afya, miundombinu n.k.

14. Mfano mzuri unajitokeza katika sekta ya elimu. Pamoja na mafanikio mengine katika sekta hii, idadi ya wanafunzi wa shule za msingi imeongezeka kutoka milioni tatu na nusu mwaka 1995 na kufikia zaidi ya milioni saba na nusu mwaka 2005. Wakati huo huo wanafunzi wa shule za sekondari wameongezeka zaidi ya maradufu kutoka wanafunzi 190,000 mwaka 1995 hadi wanafunzi 520,000 mwaka wa 2005.

15. Mafanikio katika sekta ya elimu ni kielelezo cha mafanikio katika sekta pana ya huduma za jamii. Kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu kimetoa mifano mizuri ya mafanikio katika sekta ya afya; kwa mfano upatikanaji wa dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali umeongezeka sana kwa vile kiasi cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa kimeongezeka kutoka shilingi bilioni 10 mwaka 2000 hadi shilingi bilioni 30 mwaka 2004/05. Aidha, huduma za chanjo kwa watoto zimeimarika na kuongezeka kutoka asilimia 30 mwaka 1995 hadi asilimia 90 mwaka 2004. Pia Wilaya zote zimepatiwa *X-ray, ultra-sound machine* na majokofu mapya.

16. Serikali ya Awamu ya Tatu itakumbukwa pia kwa kazi nzuri iliyoifanya katika sekta ya maji kwa kupanua na kuongeza upatikanaji wa maji nchini na pia kwa kuanzisha miradi mikubwa ya maji kama ule wa kutoa maji ya Ziwa Victoria na kuyapeleka katika mkoa wa Shinyanga, mradi wa Maji wa Chalinze katika Mkoa wa Pwani na mradi wa Maji wa Dodoma Mjini.

17. Kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tatu ni jukwaa litakaloiwezesha Serikali ya Awamu ya Nne kusimama na kuchupa ikiongozwa na Ilani ya CCM ya 2005-2010 kuelekea mafanikio makubwa zaidi ya maendeleo ya uchumi na jamii ya nchi yetu na watu wake.

# SURA YA PILI

## KUJENGA MSINGI WA UCHUMI WA KISASA WA TAIFA LINALOJITEGEMEA

***"Lazima tukimbie wakati wenzetu (walioendelea) wanatembea"***

*Mwl. J.K. Nyerere*

18. Mwelekeo wa Sera za CCM Katika Miaka ya 2000 Hadi 2010 umeainisha majukumu makuu mawili ya nchi yetu katika kipindi hiki iwapo tunadhamiria kuondokana na hali ya uchumi wetu kuwa nyuma na tegemezi. Majukumu hayo ni:

(a) Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea; yaani **modenaizesheni** ya uchumi.

(b) Kutekeleza Sera ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi.

19. Majukumu haya mawili yaliyoainishwa na Mwelekeo wa Sera za CCM Katika Miaka ya 2000 Hadi 2010 yamekuwa yakitekelezwa tangu mwaka 2000 kupitia Ilani ya Uchaguzi ya 2000 hadi 2005. Ndiyo maana kwa kuzingatia malengo hayo, Serikali imebuni mikakati ifuatayo:-

(a) Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania **(MKUKUTA).**

(b) Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania **(MKURABITA).**

(c) Mkakati wa Uanzishaji wa Maeneo Maalumu ya Uchumi (***The Special Economic Zones Strategy***)

20. Mikakati yote hii ni sehemu ya Ilani hii ya 2005-2010 ambayo inazingatia pia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Malengo ya Milenia ya Kimataifa.

21. Uchumi wa kisasa ni uchumi unaoendeshwa kwa maarifa, yaani sayansi na teknolojia. Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa maana yake ni kuanzisha mchakato wa modenaizesheni katika uchumi.

22. Mchakato wa kuitoa nchi yenye uchumi ulio nyuma na tegemezi kama ilivyo Tanzania kuelekea kwenye uchumi wa kisasa lazima uzingatie vipaumbele vikuu vitatu. Kwanza lazima **kuwaandaa kwa elimu, maarifa na mwelekeo** watu wenyewe. **Rasilimali watu** ndiyo nyenzo kuu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa. Uchumi wa kisasa hauwezi kujengwa na watu waliojikita katika mitazamo ya kijadi. Lazima wawe watu waliotayari kujifunza maarifa mapya na tabia mpya zinazoendana na matakwa ya mapinduzi ya kilimo na viwanda na pia masuala ya afya, n.k. Ndiyo maana katika mchakato wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa elimu ni lazima ipewe kipaumbele cha kwanza; elimu ya kawaida, elimu ya ufundi na elimu ya watu wazima yenye manufaa.

23. Jambo la pili la kipaumbele katika mchakato wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea ni kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Kilimo ndicho msingi wa uchumi, kwa hivyo, mapinduzi ya kilimo (pamoja na ufugaji na uvuvi) yanategemea hali halisi ya kila nchi. Kwa nchi kama Tanzania ambako wakulima wake walio wengi hawazijui kanuni za kilimo bora za mazao wayalimayo na kilimo chenyewe kinategemea jembe la mkono, kufanikiwa kuwafundisha wakulima kanuni za kilimo cha mazao wanayoyalima na wakatekeleza, jambo hilo ni la mapinduzi makubwa maana kitendo hiki peke yake kinaweza kuwaongezea mavuno kwa ekari moja mara mbili ya wavunavyo sasa na hata zaidi. Aidha, kufanikiwa kueneza matumizi ya plau za kuvutwa na maksai kwa asilimia themanini ya wakulima wetu katika miaka mitano ijayo kitakuwa kitendo cha mapinduzi makubwa. Tukifikia kiwango hicho itawezekana kuongeza wastani wa ukubwa wa mashamba ya kaya ya sasa zaidi ya maradufu.

24. Mapinduzi katika kilimo ni changamoto kubwa katika mchakato wa kujenga uchumi wa kisasa kwa sababu kubwa tatu. Kwanza mapinduzi ya kilimo yanaongeza sana ufanisi na tija katika uzalishaji na hivyo kuongeza mavuno kwa wingi. Pili, mazao ya kilimo ni

mazao ya biashara, kwa hiyo ongezeko la mavuno linawawezesha wakulima kufaidika kutokana na kuuza ziada kubwa zaidi kwenye soko na nchi inafaidika kwa kuuza mazao mengi zaidi nchi za nje. Tatu, mapinduzi katika kilimo yanaunda mazingira muafaka kwa ujio wa mapinduzi ya viwanda kwa vile hali hii itavutia uanzishaji wa viwanda vya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za viwandani kutokana na mazao ya kilimo.

25. Jambo la tatu la kipaumbele katika mchakato wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea ni mapinduzi ya viwanda na miundombinu ya kisasa. **Viwanda ndivyo kiongozi wa uchumi wa kisasa**. Dhana ya viwanda inakumbatia moja kwa moja dhana ya sayansi, teknolojia na uhandisi. Viwanda vina nafasi ya kimkakati katika mchakato mzima wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Mambo yafuatayo ni muhimu yazingatiwe:-

(i) Mapinduzi ya kilimo hayawezi kuwa endelevu bila ya mchango wa sekta ya viwanda; zana muhimu za kilimo hutengenezwa viwandani k.m. plau, trekta, mashine za kuvuna, mashine za kukoboa na kusagisha, n.k.

(ii) Mbolea na madawa hutengenezwa viwandani.

(iii) Mazao muhimu ya kilimo husindikwa na kutengenezwa viwandani na kuongezewa thamani.

(iv) Viwanda mama hutengeneza mashine, mitambo, injini mbalimbali, n.k

(v) Sekta ya viwanda ni sekta itoayo ajira zenye michepuo aina aina ya taaluma na ni uwanja wa kushamiri kwa sayansi na teknolojia.

26. Kuutoa uchumi wetu kutoka kwenye hali ya uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuuingiza kwenye mkondo wa uchumi wa kisasa, hili ndilo jukumu kuu (*central task*) la sasa. Mapinduzi ya kilimo na mapinduzi ya viwanda ndizo pande mbili za sarafu ya kujenga msingi

wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Mapinduzi ya kilimo na ya viwanda; yote yana sifa zinazofanana kiuchumi; yote yana uwezo mkubwa wa **kuongeza uzalishaji** kwa vile yanaongeza **ufanisi na tija** katika uchumi. Ziada kubwa katika uchumi ndiyo inayoleta **ukuaji mkubwa** wa uchumi. Kwa kukuza uchumi tunajijengea uwezo wa kuutokomeza umaskini.

27. Aidha, nchi yetu inahitaji ongezeko kubwa la mazao na bidhaa zinazouzwa nje ili thamani ya mapato yetu kutokana na mazao na bidhaa hizo iweze kulipia gharama ya bidhaa tunazoziingiza nchini kukidhi mahitaji mbalimbali. Hali ilivyo hivi sasa ni kuwa thamani ya mauzo yetu ya nje inaweza kulipia nusu tu ya bidhaa tunazoziagiza kutoka nchi za nje. Nusu iliyobaki ya bidhaa tunazoziingiza nchini hugharamiwa na fedha za wahisani.

28. Kwa ufupi, lazima tujenge msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Kuleta mapinduzi ya kilimo na mapinduzi ya viwanda ndizo kazi za umuhimu wa kwanza. Mambo mawili haya yakisisitizwa tutaweza katika miaka mitano ya Ilani hii kufanya mambo matatu:-

(i) Kukuza uchumi kwa kiwango cha zaidi ya asilimia kumi (10%) kwa mwaka ifikapo 2010 kutoka ukuaji wa sasa wa asilimia sita nukta saba (6.7%).

(ii) Kuanza kupunguza umaskini wa watu wetu kwa namna iliyo dhahiri.

(iii) Kutokana na ongezeko kubwa la thamani ya mazao na bidhaa tutakazouza nje ya nchi, tutaendeleza safari ndefu ya kujitegemea kwa kuwa na uwezo wa kulipia gharama za bidhaa tunazoziagiza toka nje zinazohitajika kusukuma maendeleo yetu.

29. Nchi za Asia zijulikanazo kama **Asian tigers** zimefanikiwa kujenga msingi imara wa uchumi wa kisasa kwa kuweka kipaumbele kwenye mapinduzi ya elimu, mapinduzi ya kilimo na mapinduzi ya viwanda na zimepata mafanikio ya kupigiwa mfano. Tujifunze kutoka nchi hizo.

# SURA YA TATU

## SEKTA ZA UZALISHAJI

### Kilimo

***(Kilimo cha kisasa ndio msingi wa uchumi wa kisasa)***

30. Kilimo ndio msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modenaizesheni ya uchumi wa Tanzania. Kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa.
Kilimo cha Tanzania kina matatizo yafuatayo:-

(a) Wakulima walio wengi hawazijui na hawazitekelezi kanuni za kilimo bora za mazao wanayoyalima hivyo kilimo chao hakina tija na mavuno yao ni kidogo.

(b) Wakulima wetu kwa wastani wanalima vishamba vidogo vidogo.

( c) Wakulima wetu wanategemea zana duni za jadi na hasa jembe la mkono.

(d) Upatikanaji wa mbegu bora na mbolea haujawa na mfumo wa uhakika na matumizi yake hayajaenea kwa wakulima.

(e) Karibu kazi zote za kilimo zinategemea nguvukazi ya binadamu hasa ya wanawake.

(f) Maji ya mvua yanaendelea kuachwa yaende baharini badala ya kuyakinga kwenye visima, malambo na mabwawa kwa matumizi ya watu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

31. Ili uchumi wa nchi yetu ukue kwa kiwango cha asilimia kumi ifikapo mwaka 2010 lazima kilimo kifikie ukuaji wa angalau asilimia ishirini ifikapo mwaka huo. Kwa lengo la kufikia kiwango hicho cha ukuaji wa kilimo ifikapo mwaka 2010, CCM itachukua hatua zifuatazo:-

(a) Itazielekeza Serikali kwa kutumia uongozi shirikishi kuwafikishia wakulima vijijini maarifa yanayohusu kanuni za kilimo bora cha mazao wayalimayo na elimu juu ya hifadhi ya udongo kwa kushirikiana na asasi za wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali n.k.

(b) Serikali zitaelekezwa kubuni mpango kabambe wa kueneza matumizi ya plau za kuvutwa na maksai nchini kote ukiondoa kule ambako mazingira hayaruhusu. Kila mkoa na kila wilaya itatakiwa kuwa na mpango wenye malengo yanayopimika kuelekea kwenye kueneza matumizi ya plau nchini kote,

(c) Kilimo cha kisasa lazima kimpunguzie mkulima na hasa mwanamke harubu ya kazi za kubeba mizigo, kutwanga, kukoboa na kusaga nafaka, n.k. CCM itazitaka Serikali kusimamia, kuwezesha na kushawishi kuenezwa kwa **utengenezaji na upatikanaji wa mikokoteni ya kuvutwa na wanyama na vinu vya kisasa vya kukobolea na kusagia nafaka.**

(d) Mbegu bora na mbolea ni pembejeo zenye umuhimu wa kwanza katika mageuzi ya kilimo na kuongeza tija. CCM katika kipindi cha Ilani hii itazitaka Serikali kuchukua hatua za dhati za kuweka utaratibu wenye uhakika wa upatikanaji wa mbegu bora na mbolea na wa kuzifikisha waliko wakulima kwa kushirikisha serikali za mitaa, vyama vya ushirika na watu binafsi. Aidha, utaratibu wa Serikali kutoa ruzuku ya mbolea utaimarishwa na kulenga zaidi kwenye kukuza uzalishaji katika kilimo kuliko manufaa ya kibiashara pekee. Vile vile, utatazamwa uwezekano wa kutoa ruzuku ya mbegu bora ili kuwavutia wakulima

wengi zaidi kuzitumia. Serikali itatakiwa kusimamia kwa karibu utekelezaji wa azma ya kurejesha utengenezaji wa mbolea nchini.

(e) Ili kilimo kitoe mchango wa uhakika katika ukuaji wa uchumi kwa kasi zaidi, Serikali zitatakiwa kuhimiza na kutoa vivutio, zawadi na tuzo kwa mikoa na wilaya ambazo wakulima wake wataweza kuongeza maradufu tija ya mazao yanayovunwa kwa eka katika kipindi cha Ilani hii. Msisitizo utawekwa kwenye mazao ya mahindi, mpunga, migomba, maharagwe na kunde, pamba, tumbaku, chai, kahawa na korosho. Njia bora ya kulitekeleza hili ni kwa kuweka taratibu za mashindano ya kilimo kati ya vijiji, kata, tarafa, wilaya na mikoa.

(f) CCM itazitaka Serikali Kuu na serikali za mitaa kutoa kipaumbele zaidi katika suala la kilimo cha umwagiliaji maji, msisitizo ukiwa kwenye miradi midogo na ya kati ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kuchimba mabwawa ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji.

(g) Serikali zitakuwa na wajibu wa kuwasaidia na kuwahimiza watu binafsi wenye uwezo wakope matrekta kwa ajili ya kuwalimia kwa malipo wakulima wadogo vijijini.

(h) CCM itazitaka Serikali kuwaandaa na kuwaeneza wanakohitajika **maafisa ugani** wa fani mbalimbali za kilimo.

(i) CCM itaona kwamba Serikali zinahimiza na kushauri juu ya umuhimu wa mazao ya kudumu kama minazi, michungwa, miembe, mifenesi, mikorosho, mibuni, michai, michikichi, n.k kwa uchumi wa kaya na wa nchi. Katika miaka mitano ijayo, CCM itahimiza zifanyike kampeni za makusudi za kaya kupanda mazao haya na watu wenye uwezo kuanzisha mashamba makubwa ya mazao haya ya kudumu.

(j) CCM itazitaka Serikali zihimize na kushawishi kupanuliwa na kuanzishwa kwa kilimo cha maua, matunda (mananasi, mapesheni, *apples*) viungo (*paprika*, vanila, pilipili, vitunguu, hiliki, pilipili manga) n.k. nchini ili kukuza biashara ya nje. Aidha, kilimo cha *artemizia* (mmea wa kutengeneza dawa ya malaria) nacho kitahimizwa.

(k) CCM itazitaka Serikali kuandaa mipango madhubuti ya kuhimiza kilimo cha mimea ya mbegu za mafuta kama ufuta, karanga, alizeti, michikichi, soya, mlonge n.k. na kushawishi ufufuaji na uanzishaji wa viwanda vya kusindika mafuta nchini.

(l) CCM itazitaka Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inatengewa si chini ya asilimia 10 ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, sambamba na lengo la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

(m) CCM itazitaka Serikali kuongeza msukumo katika kuvutia uwekezaji katika mashamba makubwa ya kilimo cha biashara.

(n) CCM itazitaka Serikali kuhamasisha na kusaidia uanzishaji wa viwanda vya usindikaji na ufungashaji (*packaging*) wa mazao ya kilimo kwa lengo la kuyaongezea thamani, kuvutia soko na kupunguza uharibikaji na upotevu.

(o) CCM itazitaka Serikali kutoa msukumo maalumu katika kumwezesha mkulima kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

(p) CCM itazitaka Serikali kuiwekea mkazo sera ya Mikoa/Wilaya kulima mazao kulingana na hali ya hewa ya eneo husika.

## Mifugo

32. Pamoja na kwamba Tanzania ina mifugo mingi sana; mchango wa mifugo kwenye uchumi wa Taifa ni mdogo. Kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuwaongezea kipato wafugaji, Serikali za CCM zitaendeleza kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia zaidi ubora kuliko wingi pekee katika ufugaji. Ili kufikia lengo hilo, hatua zifuatazo zitachukuliwa katika kipindi cha 2005-2010:-

    (a) Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongezea thamani mazao ya mifugo kama vile ukataji nyama, usindikaji wa maziwa, utengenezaji wa bidhaa za ngozi n.k.

    (b) Kuwashawishi Watanzania wale nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la bidhaa hizo.

    (c) Kufufua na kujenga mabwawa na majosho mapya kwa ajili ya mifugo.

    (d) Kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuuza sehemu ya mifugo yao ili wajipatie mapato.

    (e) Kuwahimiza wafugaji kutekeleza kanuni za ufugaji bora na kwa ujumla kuwawezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa.

    (f) Kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usioharibu mazingira, rasilimali muhimu kama ardhi na vyanzo vya maji kote nchini.

    (g) Kuendelea kukuza na kuendeleza masoko ya ndani ya mifugo na mazao yake.

(h) Kuendeleza mikakati ya kukuza Sekta ya Mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho.

(i) Kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe na mifugo mingine na kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mbegu hizo.

(j) Kuendelea kutenga maeneo ya wafugaji kwa lengo la kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

(k) Kuendelea kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji.

**Uvuvi**

33. Katika kipindi kijacho cha 2005-2010, Serikali za CCM zitazidisha mkazo katika kuzitumia maliasili zilizomo katika bahari, maziwa na mito ili wavuvi watumie fursa zake kuinua hali zao za maisha. Ili kufikia lengo hilo, Serikali zitaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuwasaidia wavuvi kutumia maarifa ya kisasa ya uvuvi ili kuongeza ufanisi na mapato yao.

(b) Kuwaelimisha na kuwahamasisha wavuvi wadogo kuimarisha na kuanzisha SACCOS ili ziwasaidie kupata mikopo.

(c) Kutengeneza mazingira mazuri yatakayosaidia upatikanaji wa zana za kisasa za uvuvi bila ya vikwazo.

(d) Kuvutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika samaki, hasa katika ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi na Visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia.

(e) Kushawishi sekta binafsi kuanzisha viwanda vya zana za uvuvi.

(f) Serikali za vijiji na mitaa zitahimizwa kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kupambana na uvuvi haramu.

(g) Msukumo maalumu utatolewa katika ufugaji wa samaki katika mabwawa.

(h) Kuendeleza programu mahususi ya kuzalisha na kusambaza mbegu bora za samaki.

(i) Kuimarisha na kuendeleza kilimo cha mwani.

## Wanyamapori na Misitu

34. Umuhimu wa wanyamapori na misitu unazidi kuongezeka siyo tu katika kuvutia watalii, bali pia katika kutunza mazingira. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2005–2010), Serikali chini ya CCM zitachukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili kwa manufaa ya Taifa letu.

(b) Kuzipa serikali za mitaa nguvu zaidi na kuwawezesha wananchi kumiliki na kunufaika na maliasili.

(c) Kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara.

(d) Kuvutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika asali na nta.

(e) Kuhimiza miji ianzishe bustani za ufugaji wa wanyamapori (*zoos*) kwa maonyesho.

(f) Kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji wa miti, uvunaji na udhibiti wa myoto. Ushirikishaji huo utakuwa wa sekta binafsi, NGOs na vijiji.

**Utalii**

35. Katika kipindi cha 2000-2005, Sekta ya Utalii ilipiga hatua kubwa katika kuimarisha vivutio vya utalii na kuitangaza Tanzania, na matokeo yake ni kuongezeka kwa kiwango kikubwa kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo cha 2005 – 2010, Serikali za CCM zitachukua hatua zifuatazo ili kuendeleza utalii kwa nguvu zaidi:-

(a) Kuwawezesha wananchi na serikali za mitaa, (mitaa, vijiji na vitongoji) kumiliki maeneo ya uwindaji yanayozunguka maeneo yao na hivyo kunufaika na shughuli za uwindaji katika maeneo hayo.

(b) Kukuza mwamko na kuendesha kampeni za kuwashawishi Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii.

(c) Kujenga chuo cha utalii ili kuimarisha mafunzo ya hoteli na utalii kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa huduma hizo.

(d) Kufanya juhudi maalumu za kutafuta masoko mapya ya utalii katika nchi zinazoinukia kiuchumi kama China na nchi nyingine za Asia.

(e) Kuandaa mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya utalii.

(f) Kulisaidia Shirika la Ndege la Tanzania ili lichukue nafasi yake ipasavyo ya kuwa Shirika la Ndege la Taifa (*national flag carrier*) kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufaidika zaidi na mapato yatokanayo na utalii.

(g) Kuhimiza wawekezaji wa ndani na wa nje kujenga hoteli za kitalii za hadhi ya nyota 3 hadi 5.

(h) Kuzitathmini hoteli na kuzipanga katika madaraja ya nyota zinayostahiki. Wakati huo huo kuhakikisha kuwa hoteli zinakuwa katika hali ya unadhifu.

(i) Kupanua wigo wa aina za utalii kwa kuendeleza utalii wenye kuhusisha utamaduni, mazingira (*eco-cultural tourism*), historia, na michezo k.v. gofu n.k.

(j) Serikali kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za kitalii zilizomo nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani.

(k) Kuimarisha chombo cha utalii kinachowezesha ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi katika masuala ya utalii (Tourism Confederation of Tanzania).

**Viwanda**

36. Katika mkakati wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa, Sekta ya Viwanda ni sekta kiongozi yenye jukumu la kubadilisha uchumi kuwa uchumi wa kisasa unaojitegemea kutoka uchumi ulio nyuma na tegemezi na viwanda vyake kueneza teknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa sekta zote muhimu zikiwamo za kilimo, maliasili n.k. Katika mtazamo huu wa msingi wa kukabili dhima ya maendeleo, malengo yafuatayo yatapewa kipaumbele:-

(a) Ukuaji wa sekta kufikia asilimia 15 ifikapo mwaka 2010.

(b) SIDO na sera yenyewe ya viwanda vidogo itatazamwa upya ili kuhakikisha inakidhi lengo kuu la kujenga msingi wa uchumi wa kisasa.

(c) Kuongeza ushiriki wa sekta isiyo rasmi na sekta ya viwanda vidogo na vya kati (SMEs) katika uzalishaji wa bidhaa.

(d) Kuendelea na ubinafsishaji na ukodishaji wa viwanda na mashirika ya umma yaliyobaki.

37. Ili kufikia malengo hayo ya jumla,CCM itazisisitizia Serikali kuchukua hatua zifuatazo :-

(a) Kuvutia wawekezaji katika ufufuaji wa viwanda vilivyopo na kujenga vipya katika sekta zilizopewa kipaumbele.

(b) Kuendelea kushirikiana na asasi mbalimbali kuboresha zaidi mazingira ya uzalishaji viwandani ikiwa ni pamoja na miundombinu, sera za fedha na kodi na kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo.

(c) Kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani mazao mbalimbali ya kilimo, mifugo, madini, uvuvi, maliasili n.k.

( d) Kuongeza uwezo wa NDC katika kuongoza juhudi za uanzishaji wa viwanda mama.

(e) Kuongeza uwezo wa SIDO katika uwezeshaji wa kitaalamu na mitaji katika sekta ya viwanda vidogo na vya kati.

(f) Kutoa umuhimu katika kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta za kipaumbele; yaani sekta ndogo za nguo, ngozi na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na vyakula; mkazo ukiwekwa katika mipango ifuatayo:-

(i) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi.

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa programu inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na chakula.

(iii) Serikali kuendeleza jitihada za kuwapata wabia wa kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na mradi wa chuma wa Liganga ndani ya mfumo wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara.

(iv) Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje (EPZ) na uwekezaji katika viwanda ndani ya maeneo hayo.

(v) Kuanzisha utaratibu wa kutenga maeneo maalumu ya kiuchumi (*Special Economic Zones – SEZs*), kwa ajili ya uzalishaji utakaolenga masoko yote ya ndani na ya nje.

(vi) Kubuni mpango wa kuandaa mabingwa katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ya viwanda.

.

(g) Serikali kutafuta wabia wa kuendeleza miundombinu ya kiufundi iliyopo nchini yenye uwezo wa kutengeneza mashine na mitambo (*machine tools*) na kukuza uwezo wa kutengeneza vipuri mbalimbali.

(h) Kulinda, kuimarisha na kutumia uwezo wa kiteknolojia uliokwishajengwa nchini kama vile katika **karakana** za TRC, TAZARA (Mang'ula) n.k.

(i) Kutafuta wawekezaji katika sekta ya kuunganisha magari, matrekta na mashine nyingine muhimu.

## Madini

38**.** Pamoja na ukuaji wa kasi wa Sekta ya Madini, mchango wake katika Pato la Taifa bado ni mdogo. Katika kipindi kijacho cha

2005-2010, malengo makuu ya Sekta ya Madini yatakuwa ni kuongeza sehemu ya madini inayosafirishwa ikiwa imeongezewa thamani kutoka asilimia 0.3 ya madini yanayosafirishwa ya sasa hadi kufikia asilimia 3.0 mwaka 2010.

39. Katika kufikia lengo hilo, Serikali za CCM zitachukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kukuza ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi katika kuweka mazingira bora ya kuvutia uwekezaji katika kuanzisha migodi mipya.

(b) Kuweka mazingira ya kuvutia wawekezaji katika miradi ya kuongezea thamani madini kama vile ukataji wa madini na utengenezaji wa vito, chini ya utaratibu wa maeneo maalum ya kiuchumi (SEZs).

(c) Kuimarisha usalama migodini.

(d) Kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo na maarifa mapya katika fani ya uchimbaji madini.

(e) Kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo.

(f) Kuendeleza utafutaji wa madini, mafuta na gesi nchini.

(g) Kuipitia upya Sera ya Madini kwa lengo la kuiboresha katika maeneo mbali mbali yakiwemo yafuatayo:-

(i) Ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi kwa njia ya hisa kwa kuzingatia rasilimali na michango ya Serikali katika utafiti na ufikishaji wa miundombinu.

(ii) Ushiriki wa Serikali na wa Watanzania katika umiliki wa migodi mikubwa kwa utaratibu wa *equity participation* na ununuzi wa hisa.

(iii) Mfumo wa vivutio kwa wawekezaji kwa lengo la kuwezesha nchi pamoja na wananchi wake kunufaika zaidi na rasilimali hii ya taifa.

(iv) Utaratibu utakaoweza kuwekwa kwa makusudi kwa lengo la kuyawezesha maeneo yanayozunguka migodi kufaidika zaidi na harakati za migodi hasa katika kurekebisha athari za kijamii na kimazingira zinazotokana na uchimbaji wa madini.

(v) Utaratibu utakaoeleweka zaidi wa fidia na makazi mapya kwa wale wanaolazimika kuhamishwa kwa ajili ya kupisha shughuli za utafiti na uchimbaji wa madini.

**Biashara na Masoko**

40. Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kipindi kilichopita za kuboresha mazingira ya uwekezaji, biashara imechangamka nchini. Ili kuyalinda na kuyaendeleza mafanikio yaliyopatikana, Serikali za CCM zitachukua hatua zifuatazo katika kipindi kijacho cha 2005-2010:-

(a) Kuweka mikakati itakayoliwezesha Taifa kuhimili ushindani wa biashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya kimataifa katika mazingira ya utandawazi.

(b) Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda (EAC, SADC) na wa kimataifa (WTO) kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji.

(c) Kuhimiza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) katika biashara.

(d) Kuweka mfumo utakaoweka mtiririko mzuri wa masoko ya ndani.

(e) Kuelimisha wananchi kuhusu hakimiliki.

(f) Kuendeleza Programu Maalumu ya Uuzaji Bidhaa Nje (*Export Development Strategy* - EDS), na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mauzo Nje (Export Development Fund - EDF).

41. Mafanikio ya mifumo bora ya masoko yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa miundombinu bora ya masoko, kupatikana kwa mitaji na mikopo, kuwepo kwa stadi za biashara, na mahusiano kati ya wadau ambayo yanaongozwa na taarifa sahihi za masoko. Kwa sababu hiyo, Serikali za CCM zitayapa kipaumbele mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao kwa walengwa.

(b) Kuandaa kitabu cha orodha ya wanunuzi na wasindikaji wa mazao (*Agri-business Directory*) na kuisambaza kwa wadau.

(c) Kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko kwa vikundi vya wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara wa kati ili waweze kuzalisha na kuuza kwa kufuata mahitaji ya soko.

(d) Kuwezesha halmashauri za miji na wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kutunza taarifa za masoko katika maeneo yao.

(e) Kutoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko na biashara na nchi za nje hususani nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na nchi nyingine ambazo zinatoa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zinazoendelea.

(f) Kuandaa mikakati ya kuendeleza soko la ndani.

(g) Kuratibu na kufanya tathmini ya ubora wa miundombinu ya masoko.

(h) Kuweka mfumo utakaowezesha matumizi ya maghala kama dhamana ya kukopea.

(i) Kuhimiza matumizi ya maghala kwa kuhifadhia mazao ya wakulima kama mkakati wa kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

# SURA YA NNE

## SEKTA ZA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA KIUCHUMI

### Ardhi

42. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kwamba ardhi wanayomiliki wananchi ni mtaji wao wa msingi wa kutegemewa katika kuwapatia ajira, kuwaondolea umaskini na kuwaletea ustawi wa jamii pale walipo. Chama pia kinatambua kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na kupunguza kero za ardhi na makazi na kutoa elimu na miongozo kuhusu kumiliki ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi. Ili mafanikio hayo yaendelee kuwa chachu ya maendeleo mijini na vijijini katika miaka mitano ya 2005 - 2010, Chama kitahimiza Serikali kuhakikisha kuwa hatua zifuatazo zinachukuliwa:-

    (a) Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (**MKURABITA)** kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya mabenki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha. Aidha, mabenki nayo yataandaliwa ipasavyo katika kubadili tabia ili yaondokane na mawazo ya ugumu katika kutoa mikopo.

    (b) Kuendeleza kwa nguvu mpya kazi inayofanywa na halmashauri za wilaya katika kutambua mipaka ya vijiji, kupima na kuvipatia vijiji hati za kumiliki ardhi ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote;

    (c) Kuendelea kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

    (d) Kuendelea kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu na miji kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo. Aidha, uwezo wa kupata

wataalamu na vitendea kazi kwa ajili ya kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya maji, maziwa na bahari kupitia Tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba 2000, utaendelea kujengwa na kutumiwa ipasavyo.

## Nishati

43. Pamoja na hatua nyingi zilizochukuliwa kipindi cha nyuma za kuboresha upatikanaji wa nishati, bado uwezo uliopo nchini wa kupata nishati kwa wingi haujatumika ipasavyo. Aidha, umeme unaopatikana hivi sasa ni wa gharama kubwa. Katika kipindi kijacho, hatua zifuatazo zitachukuliwa zenye lengo la kuongeza nishati na hasa umeme unaozalishwa na kuongeza uhakika wa upatikanaji na usambazaji wake ili uwafikie wananchi wengi zaidi:-

(a) Kupanua wigo wa aina za vyanzo vya umeme na nishati nyingine, kwa lengo la kuzalisha umeme wa kutosha kukidhi mahitaji ya uzalishaji viwandani na matumizi ya nyumbani. Mipango/miradi ifuatayo itashughulikiwa kwa ajili ya kufikia lengo hilo na mengine:-

(i) Umeme kutokana na makaa ya mawe, Mchuchuma.

(ii) Umeme wa gesi ya Mnazi Bay kwa ajili ya mikoa ya Mtwara na Lindi.

(iii) Kufufua mipango kuhusu miradi ya umeme ya Mto Rusumo na Stiglier’s Gorge.

(iv) Kutazama uwezekano wa ukusanyaji wa takwimu za kasi ya upepo na kuanza matumizi ya nishati ya upepo kwa wingi zaidi.

(v) Kutazama uwezekano wa uzalishaji umeme kutokana na mabaki ya mkonge, miwa na ya mazao mengine.

(vi) Kuweka mazingira yatakayorahisisha matumizi ya nishati mbadala ya kuni vijijini kama vile nishati ya jua (umeme nuru) na *biogas*.

(b) Kufikisha umeme katika miji mikuu ya Wilaya za Bukombe, Kilindi, Simanjiro, Kibondo, Kasulu, Mbinga na Tunduru na kuanza hatua za kuipatia umeme miji mikuu ya Wilaya nyingine mpya.

(c) Kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini utakaoshirikisha sekta binafsi na wahisani.

(d) Kuweka mkakati wa uzalishaji umeme wa kutosha na wa gharama nafuu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi viwandani.

(e) Kuiunganisha Mikoa ya Kigoma na Ruvuma na gridi ya Taifa.

(f) Kuendelea kutafuta wawekezaji wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

(g) Kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa umeme.

(h) Kuendelea kutafuta mafuta kwa kasi zaidi.

(i) Kuanzisha mradi wa gesi kwa matumizi ya nyumbani kutokana na gesi ya Songosongo kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni na mkaa majumbani.

**Barabara**

44. Kipindi cha Awamu ya Tatu kimeshuhudia ujenzi na uboreshaji mkubwa wa barabara nchini. Katika kipindi cha miaka mitano cha 2005-2010, Serikali chini ya uongozi wa CCM zitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara (Tanzania Road Fund).

(b) Kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambao unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika barabara kuu.

Barabara hizo ni Dodoma-Manyoni, Manyoni-Singida, Singida-Shelui, Shelui-Igunga, Igunga-Nzega-Ilula; Muhutwe-Kagoma; Nangurukuru-Mbwemkulu-Mingoyo; Mkuranga-Kibiti; Pugu-Kisarawe; Chalinze-Morogoro-Melela; Tunduma-Songwe; Kiabakari-Butiama; Dodoma-Morogoro; Kagoma-Biharamulo-Lusahunga; Tabora-Kaliua-Malagarasi- iUvinza- Kigoma; Usagara-Chato-Biharamulo na Ndundu-Somanga.

(c) Kuendelea kuimarisha barabara nchini zitakazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami; zitakazounganisha Makao Makuu ya Mikoa yote pia kwa barabara za lami na kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya zote kwa barabara zinazopitika wakati wote;

(d) Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo:-

Tunduma-Sumbawanga;Marangu-Tarakea-Rongai; Minjingu-Babati-Singida; Rujewa-Madibira-Mafinga; Mbeya-Chunya-Makongolosi; Msimba-Ikokoto-Mafinga; Arusha-Namanga; Tanga-Horohoro; na ukarabati wa Barabara ya Kilwa (DSM), Barabara ya Mandela (DSM) na Barabara ya Sam Nujoma (DSM).

(e) Kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu barabara zifuatazo kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami: Maganzo-Maswa-Bariadi-Mkula-Lamadi; Babati-Dodoma-Iringa; Sumbawanga-Kigoma-Nyakanazi; Musoma-Fort-Ikoma; Korogwe-Handeni-Kilosa-Mikumi; Nzega-Tabora-Sikonge-Chunya; Mtwara-Masasi-Songea-Mbamba Bay;

Manyoni-Itigi-Tabora; Ipole-Mpanda-Kigoma na Bagamoyo-Saadani.

(f) Kuhimiza maandalizi na ujenzi wa Daraja la Kigamboni chini ya uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam;

(g) Kuhakikisha upatikanaji wa kivuko kipya cha Kigongo-Busisi (Mwanza);

(h) Kukamilisha ujenzi wa daraja jipya la Mpiji ambalo litawezesha njia mbadala ya Dar es Salaam-Tanga.

(i) Kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa daraja la Mto Kilombero na kukamilisha ujenzi wa daraja la Mto Mwatisi katika Mkoa wa Morogoro.

(j) Kufanya usanifu wa daraja jipya la Ruvu;

(k) Kuendelea kuandaa mazingira mazuri ya kuishirikisha sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT).

(l) Kuanza ujenzi wa Daraja la Umoja (Tanzania na Msumbiji).

(m) Kuanzishwa Programu ya Taifa ya Usafiri Vijijini.

## Usafiri na Uchukuzi

**(*Tanzania, lango kuu la Ukanda wa Maziwa na Kusini mwa Afrika).***

45. Kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi, Serikali chini ya CCM katika kipindi cha 2005 - 2010, itaendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na muungano wa wasafirishaji wa abiria na mizigo kupitia vyombo vyao kwa lengo la kuboresha hali ya usafiri na

uchukuzi wa barabara mikoani na vijijini, pamoja na usafiri wa majini na angani. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Pia, Shirika litaendelezwa kama muhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati.

(b) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) ili liweze kuhimili kwa uwezo mkubwa zaidii majukumu ya kuboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa mpango wa eneo la Ukanda wa Mtwara.

(c) Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha-Musoma, Isaka-Kigali na eneo la Ukanda wa Mtwara ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara, Songea, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga.

(d) Kuimarisha Bandari za Kigoma na Kasanga.

(e) Kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa. Aidha, uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari.

(f) Kuendelea kuutengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam yatakayoweza kuundeleza kuwa kiungo (*hub*) cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa.

(g) Kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuimarisha Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga.

(h) Kutekeleza mradi wa mabasi ya usafiri wa haraka jijini Dar es Salaam.

**Mawasiliano**

46. Sekta ya mawasiliano ni miongoni mwa sekta zilizoshuhudia mabadiliko makubwa katika kipindi kilichopita. Katika kipindi cha 2005 -2010 Chama Cha Mapinduzi kitazihimiza Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuboresha mtandao na huduma za simu nchini.

(b) Kuendelea kupanua huduma za simu za mezani na za mkononi hadi ngazi ya vijiji.

(c) Kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi. Aidha, kuimarisha na kupanua mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta.

(d) Kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha mfuko maalum wenye lengo la kupeleka huduma za simu na *internet* hadi vijijini.

(e) Kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano kikanda na kimataifa (*ICT hub through marine optic fibre system*).

(f) Kuimarisha uwezo wa utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vya kisasa.

**Sekta ya Fedha**

47. Sekta ya Fedha ni huduma ya kiuchumi ambayo ni mwezeshaji mkuu siyo tu wa shughuli za kiuchumi, bali pia hata za miundombinu. Kupanuka na kuendelea kwa Sekta ya Fedha kumechangia kwa kiasi kikubwa katika kuchangamsha biashara na kukua kwa uchumi. Katika kipindi cha 2005-2010, Sekta ya Fedha itaendelea kuimarishwa ili iweze kukabili ipasavyo changamoto ya huduma na kupanuka kwa uchumi wa Taifa. Miongoni mwa mambo yatakayoshughulikiwa ni suala la riba za mabenki kwa mtazamo wa kupunguza tofauti kubwa baina ya riba za kukopeshea na riba za kukopea. Lengo ni kuweka mazingira mazuri ya kujenga tabia ya kujiwekea akiba miongoni mwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo.

*"**Uchumi wa soko hauwezi kushamiri iwapo wananchi walio wengi si washiriki....**Mkakati mmojawapo, ambao tayari tunaushughulikia, ni wa kutambua rasmi rasilimali na biashara za wanyonge ambazo bado ziko kwenye sekta isiyo rasmi ili zitumike kuwafanya wawe washiriki kamili kwenye uchumi rasmi wa taifa."*

*Ndugu Benjamin William Mkapa*
*Mwenyekiti wa CCM*
*25 Agosti, 2004*

# SURA YA TANO

## SERA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

***"Lengo letu ni kusukuma ukuaji wa uchumi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya"***

***Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete,***
***Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano***
***Wa Tanzania kwa tiketi ya CCM***

48. Lengo la Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ya CCM ni kuona kwamba wananchi wa Tanzania wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao. **Sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi** imebuniwa kama njia ya uhakika ya kuwapa Watanzania uwezo na fursa ya kulifikia lengo hilo la kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi. Aidha, Sera hii ina lengo la kuona kwamba Watanzania kwa mamilioni wanashiriki kwa ukamilifu katika harakati za kukuza uchumi wetu na kuondoa umaskini (MKUKUTA). Wakati huo huo, utekelezaji wa dhati wa sera hii ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi itatuepusha na balaa la kuwa na jamii ambayo ina **matajiri wachache walionacho na wananchi walio wengi wasio nacho.**

49. Ili utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ifanikiwe, CCM inatoa wito kwa Watanzania kudhamiria yafuatayo:

(a) Kwanza kukubali kuwa kujitegemea kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa ndio msingi wa maendeleo na kutokomeza umaskini.

(b) Kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi ana wajibu wa kujiwezesha kwa kuishi kwa jasho lake, yaani kwa kufanya kazi.

(c) Mtaji wa maskini ni nguvu (na akili) zake mwenyewe. Uwezeshaji ni njia ya kumuunga mkono.

50. Watanzania walio wengi hawakupata nafasi ya kuendeleza vipaji vyao au kuwa na mali au nyenzo za kuzitumia katika kujiendeleza kimaisha. Katika miaka mitano ya Ilani hii CCM itazielekeza Serikali kuweka mipango ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kujiendeleza kimaisha. Mipango ya uwezeshaji itakuwa pamoja na ifuatayo:

(a) ***Elimu na Mafunzo***: Watu wetu wengi wanashindwa kujitegemea na kujiendeleza kiuchumi kwa kuwa na elimu ndogo au maarifa na ujuzi mdogo. Elimu ya kawaida na mafunzo ya ufundi stadi na maarifa ya kazi ni uwezeshaji wa msingi sana kwa binadamu. Serikali zitaimarisha mipango ya elimu ya watu wazima yenye manufaa pamoja na mafunzo ya fani mbalimbali za stadi za kazi mijini na vijijini. Mafunzo haya yatahusu kilimo, biashara, ufugaji, utunzaji wa vitabu, n.k. Serikali zitaongoza shughuli hizi za kutoa elimu na maarifa ya kazi kwa wananchi zikishirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali.

(b) ***Ushirika na Uwezeshaji:*** Ushirika ndio njia kuu ya uwezeshaji kwa wananchi walio wengi. Ushirika ni njia ya kukusanya nguvu. Ushirika uko wa aina nyingi. Lakini **ushirika wa kuweka na kukopa** una umuhimu wa kimkakati katika harakati za kukuza uchumi na kutokomeza umaskini kwa sababu unawawezesha wanachama wa ushirika huo kuwa na chombo chao cha kuwapatia mikopo (mitaji) kwa uhakika na kwa masharti nafuu.

Aina nyingine za ushirika ni pamoja na ushirika wa wakulima wa mazao na mifugo, ushirika wa biashara, ushirika wa huduma kama migahawa, ushirika wa wavuvi, ushirika wa wachimba madini, ushirika wa ujenzi, n.k.

Kwa vile ushirika ndiyo njia kuu ya uwezeshaji wa wananchi, CCM itazisisitizia Serikali juu ya **umuhimu wa kuandaa maafisa wa ushirika waadilifu, wataalamu na wenye uzalendo.**

(c) Serikali imebuni utaratibu wa kuzipa uhai wa kisheria ardhi na nyumba ambazo hadi sasa hazikutambuliwa kisheria. Kwa utaratibu huu wenye ardhi na nyumba hizi wanaweza kupata mikopo kwa kuweka ardhi na nyumba hizo dhamana. Utaratibu huu unaitwa **MKURABITA**, yaani Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania. Lengo lake ni kuwafanya wananchi waliokuwa hawakopesheki sasa wakopesheke na hivyo kuingia katika mchakato wa uchumi hai.

(d) ***Uwezeshaji wa Mitaji***: Wananchi wengi wana uwezo, maarifa na dhamira ya kujitegemea kiuchumi. Mipango mizuri ya mikopo ya masharti nafuu inaweza kuwafanya wengi wao wakajiajiri na hivyo kuboresha maisha yao na kutoa mchango katika uchumi wa taifa. Shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini, biashara, n.k. zinaweza kushamiri iwapo utakuwapo utaratibu madhubuti wa mikopo yenye masharti nafuu. Upatikanaji wa mitaji kwa njia ya mikopo ni kikwazo kikubwa kwa watu wengi. Serikali za CCM ziwajibike katika kuweka mfumo muafaka wa mikopo kwa wananchi.

(e) ***Uwezeshaji kwa Kubadilishana Uzoefu****:* Kuna fani za shughuli za kiuchumi ambazo Watanzania hatuna uzoefu nazo. Fani mojawapo ni ya **ujasiriamali.** CCM itazishauri Serikali kuwa na mipango ya kuwapa fursa wajasiriamali Watanzania wanaoinukia kupata uzoefu wa wajasiriamali wa nchi nyingine za Kusini. Aidha, katika madarasa ya ujasiriamali na biashara, mifano halisi ya mafanikio katika nchi nyingine itatolewa kama mifano.

(f) ***Kuwawezesha wafugaji:*** Kuwapa elimu ya ufugaji wa kisasa na kuwatanabahisha kuwa mifugo ni mali; waitumie ili kuboresha hali ya maisha yao.

***AJIRA NA UWEZESHAJI WA WANANCHI***

51. CCM imekisikia na kukipokea kilio cha ajira cha wananchi, hasa vijana. CCM inaahidi kulipa suala la ajira umuhimu mkubwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Lengo la CCM ni kuona kwamba ajira mpya zaidi ya milioni moja zinapatikana katika miaka mitano ijayo.

(a) Ajira ziko za aina mbili:

i) Ajira katika maana ya kazi ya kulipwa mshahara katika sekta ya umma (Serikali na vyombo vyake) na katika sekta binafsi (iliyo rasmi na isiyo rasmi).

ii) Ajira katika maana ya kujiajiri binafsi – katika kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, biashara, kuchimba madini, udereva, ufundi, ualimu, uhasibu, kuendesha mgahawa, ushonaji, uandishi, uanasheria, uhandisi, ukandarasi n.k.

( b) Nafasi za ajira katika sekta ya umma zinapatikana lakini kwa sharti la ikama, taaluma na uwezo wa bajeti. Hata hivyo, katika miaka mitano ijayo, pamoja na nafasi za ajira zitakazotokana na watu kustaafu na kufariki, kutakuwa na ajira mpya nyingi kwenye sekta ya ualimu kutokana na upanuzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu unaoendelea. Sekta ya afya pia itatoa ajira mpya nyingi kwa upande wa waganga na wauguzi kwa vile sekta hii lazima ipanuke kukidhi mahitaji ya wananchi. Sekta ya ujenzi vile vile ina nafasi ya kutoa ajira mpya nyingi.

(c) Serikali za CCM zitahimizwa kuendelea kuvutia wawekezaji katika viwanda, migodi, kilimo, n.k. ili nafasi za ajira ziendelee kuongezeka. Mkakati mpya wa Serikali wa kuanzisha maeneo maalum ya uchumi (SEZs) umekusudiwa kuibua nafasi nyingi mpya za ajira.

(d) **Eneo la kujiajiri** ndilo lenye **nafasi tele za ajira** katika nchi yetu. Katika kipindi cha Ilani hii, CCM itazihimiza Serikali zielekeze nguvu zake kwenye kuwawezesha wananchi, hasa vijana na wanawake, kwenye shughuli za kujiajiri vijijini na mijini.

(e) CCM inatoa wito kwa wananchi wajitokeze kuitikia wito wa kujiajiri na pia wakubali **kutobagua kazi** maana wahenga wamesema **mchagua jembe si mkulima**.

(f) CCM itazielekeza Serikali kuona kwamba mipango ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inaandaliwa kwenye kila Wilaya. Kila Wilaya ina rasilimali za kutosha, mradi tu watu wanaamua kuibua maendeleo yao. Mchango wa fedha (kwa ajili ya mikopo) kutoka Serikali Kuu na wa taasisi zisizo za Kiserikali inakusudiwa upelekwe Wilayani huko huko.

(g) Serikali zitatakiwa kuzielekeza Ofisi za Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya na Ofisi za CCM za Wilaya (Idara ya Uchumi na Fedha) zijijengee uwezo wa kuwashauri wananchi wanaoomba mikopo kuhusu maandalizi ya michanganuo ya miradi inayokubalika.

***MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII NA UWEZESHAJI KIUCHUMI***

52. Pamoja na suala la kukaribisha wawekezaji nchini ili kukuza uchumi na kuongeza ajira, kuna umuhimu wa kufikiria uwezekano wa kuutumia uwezo mkubwa wa fedha uliopo katika mashirika ya hifadhi za jamii (pensheni) yaani NSSF, PPF, LAPF na Mfuko wa Pensheni ya Serikali. Tayari NSSF na PPF wameweza kuwekeza katika miradi ya nyumba (k.m. NSSF wamejenga mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mabibo) na kusaidia kutatua matatizo makubwa ya kijamii.

53. CCM itaelekeza Serikali kufanya mashauriano ya msingi na uongozi wa mifuko hii ili kupata njia muafaka za kuifanya mifuko hii

ishiriki katika uwekezaji na hivyo kuliongezea nguvu taifa ya kukuza uchumi wake kwa kasi zaidi. Utaratibu wa kuitumia mifuko ya hifadhi ya jamii kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa nchi unatumika sana katika nchi za Magharibi ikiwemo Uingereza. Afrika ya Kusini pia ina uzoefu huo.

### *HARAMBEE ZA KUWEZESHANA KATIKA KUPAMBANA NA UMASKINI*

54. Watanzania wa asili mbalimbali wana jadi ya kuungana mkono kwa hali na mali, kuchangiana na kusaidiana kwa msingi wa udugu, urafiki, utani, ujirani, n.k. Tabia ya watu kuungana mkono (*solidarity*) ni nzuri na inafaa ikaendelezwa lakini kwa kupewa mrengo wa kimaendeleo.

55. CCM katika kipindi cha Ilani hii itawahimiza Watanzania kuandaa na kuendesha harambee za kuwawezesha ndugu, marafiki na jirani waliopungukiwa uwezo wa kuwasomesha watoto wao au watoto yatima. Zinaweza kuandaliwa pia harambee ili kumwezesha ndugu, rafiki au jirani kupata matibabu muhimu kwa vile yeye mwenyewe hana uwezo wa kumudu gharama hizo.

56. Hadi sasa wananchi wengi wanaendesha harambee (michango) kwa malengo ya mambo ya sherehe kama harusi, ngoma, n.k. Wakati sasa umefika kwa jamii zetu kujielekeza kwenye michango (harambee) ya kuwezeshana katika fani za elimu, afya na uchumi kwani hizi ni nyenzo za msingi katika kupambana na umaskini.

# SURA YA SITA

## SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

57. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa **rasilimali watu** ndiyo nyenzo kuu ya maendeleo yote ya nchi. Watu walioelimika na wenye afya ndio chombo na lengo la harakati za kukuza uchumi na kuutokomeza umaskini. Ndiyo maana katika harakati za taifa za kuondokana na uchumi ulio nyuma na tegemezi suala la elimu bora ya aina na fani zote na la huduma bora za afya kwa wananchi wetu linapewa umuhimu wa kwanza.

### Elimu

58. CCM katika kipindi cha 2005-2010 itazielekeza Serikali kuendelea kushirikiana na wahisani, mashirika ya dini, sekta binafsi na wananchi kwa jumla katika kuimarisha elimu katika ngazi mbali mbali.

### *Elimu ya Awali*

59. Lengo la CCM kwa kipindi cha 2005-2010 ni kuongeza kasi ya upanuzi wa elimu ya awali kwa kuhamasisha sekta binafsi na kuhakikisha kwamba sera ya kila shule ya msingi kuwa na darasa la elimu ya awali inatekelezwa ipasavyo**.**

### *Elimu ya Msingi*

60. Baada ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa MMEM, CCM katika kipindi cha 2005-2010 itazielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

    (a) Kuongeza kiwango cha ubora wa elimu.

    (b) Kuweka msukumo maalum wa uandikishaji wa watoto wote wa rika lengwa la watoto wa umri wa miaka 7-13 (NER) katika ngazi ya elimu ya msingi kufikia asilimia 100

mwaka 2010. Aidha, kuongeza uandikishaji wa watoto wenye ulemavu na wengine wenye matatizo maalumu.

(c) Kuendelea kujenga na kupanua miundombinu ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu, madarasa, vyoo na huduma zinazohusika.

(d) Kuendelea kuhakikisha kwamba maslahi ya walimu yanaboreshwa na kulipwa kwa wakati.

(e) Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shule ili kuimarisha ubora wa elimu.

(f) Kuongeza idadi ya wanafunzi watakaoendelea na elimu ya sekondari kufikia asilimia 50 ya watahiniwa wa Darasa la Saba ifikapo mwaka 2010.

***Elimu ya Sekondari***

61. CCM itazielekeza Serikali kuchukua hatua za kuendeleza elimu ya sekondari katika kipindi cha 2005 - 2010 kama ifuatavyo:-

(a) Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

(b) Kuendelea kutekeleza azma ya kuwa na angalau shule moja ya sekondari kwa kila Kata.

(c) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Kidato cha 1-4 kufikia asilimia 50 ya watoto wa rika lengwa la umri wa miaka 14-17 ifikapo mwaka 2010.

(d) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Kidato cha 5-6 kufikia asilimia 25 ya vijana wa rika lengwa la umri wa miaka 18-19 ifikapo mwaka 2010.

(e) Kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari na kuongeza viwango vya kufaulu katika Kidato cha 4 na cha 6.

(f) Kujenga nyumba za walimu na kuendelea kuboresha maslahi yao.

***Elimu ya Ualimu***

62. Katika kipindi cha 2005 - 2010, mafunzo ya ualimu yataendelea kupanuliwa na Serikali za CCM kwa lengo la kuwezesha shule za msingi na sekondari kuwa na walimu wa kutosheleza mahitaji na wenye kutimiza sifa zote zitakiwazo. **Pia suala la kuandaa walimu wa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi litashughulikiwa kama mkakati wa kukieneza Kiswahili.** Miongoni mwa hatua mahususi zitakazochukuliwa katika kutekeleza dhamira hizo ni:-

(a) Kuona kwamba vyuo vikuu vishiriki viwili vya elimu vya Mkwawa na Chang'ombe vinaanzishwa. Aidha, chuo cha Walimu cha Mtwara kitafanywa kuwa chuo kiambata (*associate college)*.

(b) Katika vyuo na vyuo vikuu mbalimbali vya walimu, idadi ya walimu tarajali wa lugha ya Kiswahili itaongezwa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya ndani na ya nje ya nchi.

***Elimu ya Juu***

63. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itazielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi washiriki kwa ukamilifu kuwekeza katika elimu ya juu na kuchangia elimu hiyo kupitia Mfuko wa Elimu.

(b) Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu kwa lengo la kuwezesha asilimia 12.5 ya wanaomaliza Kidato cha 6 kupata nafasi za kuendelea na masomo katika vyuo

vikuu, taasisi za teknolojia na taasisi nyingine za elimu ya juu.

(c) Kuendelea kuhamasisha wanafunzi wa kike kuchukua masomo ya sayansi.

(d) Kuweka utaratibu wa kutumia Mfuko wa Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili wanafunzi wengi zaidi waweze kufaidika na Mfuko huo.

(e) Kuendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu.

(f) Kuendelea kuimarisha vyuo vya elimu ya juu vya ufundi na kuanzisha mtandao wa taasisi za sayansi na teknolojia.

(g) Kuimarisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kivukoni.

(h) Kuhakikisha kuwa mitaala ya elimu ya juu inakidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na kujiajiri.

***Mafunzo ya Ufundi Stadi***

64. Serikali chini ya CCM katika kipindi hiki zitaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuongeza kasi ya upanuaji wa mafunzo ya ufundi stadi na kuishirikisha sekta binafsi.

(b) Kuanzisha Vyuo vya VETA angalau kimoja kwa kila wilaya kwa lengo la kuongeza nafasi za masomo ya ufundi stadi.

## ***Elimu ya Watu Wazima***

65. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itazihimiza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

    (a) Kufufua mpango wa awali wa elimu ya watu wazima.

    (b) Kuendelea kuboresha elimu ya watu wazima kwa kutumia mbinu shirikishi ya "*reflect*" ambapo walengwa wanajifunza kusoma, kuandika na kuhesabu kwa namna inayowasaidia kujiongezea ujuzi katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

    (c) Kuimarisha Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Walioikosa (MEMKWA).

## **Afya**

66. Utoaji wa huduma ya afya umeboreshwa kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha Awamu ya Tatu. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itaendelea kuhimiza Serikali zake kuchukua hatua zifuatazo:-

    (a) Kuongeza jitihada katika kupambana na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu yanayojitokeza mara kwa mara. Mikakati ya kinga itapewa kipaumbele hususani kuendelea kuweka msisitizo zaidi kwenye **kinga kuliko tiba.**

    (b) Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka watoto 95 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai (kwa utafiti wa mwaka 2002) hadi 50 mwaka 2010.

    (c) Kupunguza vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka 5 kutoka 154 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai (kwa utafiti wa mwaka 2002) hadi 79 mwaka 2010.

(d) Kupunguza vifo vya uzazi kutoka 529 kati ya wazazi 100,000 (kwa utafiti wa mwaka 2002) hadi 265 mwaka 2010.

(e) Kuongeza kiwango cha wazazi wanaozalishwa na wakunga waliopata mafunzo kutoka asilimia 50 (kwa utafiti wa mwaka 2002) hadi asilimia 80 mwaka 2010.

(f) Kuimarisha vita dhidi ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutumia vizuri misaada ya wahisani na **kuelimisha wananchi dhidi ya unyanyapaa**. Jitihada za kufikisha elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa wananchi mitaani na vijijini ziongezwe. Mpango wa kutoa dawa za kurefusha maisha na kupunguza makali kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI utaimarishwa.

(g) Kukamilisha mipango itakayowezesha huduma za upasuaji wa moyo kutolewa humu humu nchini.

(h) Kuhakikisha kuwa huduma za bima ya afya zinawafikia Watanzania wengi zaidi badala ya asilimia 3 tu ya sasa.

(i) Kukamilisha ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

(j) Kuendelea kuzipatia vifaa vya kisasa hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali.

**Maji**

67. Kutokana na umuhimu wa maji, Serikali chini ya CCM katika kipindi cha 2005-2010 zitaendelea kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na kusisitiza yafuatayo:-

(a) Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya

kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakaazi wa mijini na asilimia 65 ya wakaazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010.

(b) Kuhimiza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, ukarabati na kufufua malambo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo.

(c) Kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zake zote za kutoa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza kamati za maji za vijiji sambamba na kuimarisha mifuko ya maji ambayo imeanzishwa na wananchi.

(d) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ni pamoja na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Shinyanga Mjini na Kahama, Mradi wa Maji wa Chalinze katika Mkoa wa Pwani na Mradi Kabambe wa Kufufua Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka Katika Jiji la Dar es Salaam.

(e) Kuhimiza, kuimarisha na kupanua teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga, kutunza na kutumia maji ya mvua.

(f) Kuandaa mazingira mazuri ya kisheria kuhusu rasilimali za maji na kubaini vyombo na muundo utakaomudu majukumu, mipango na menejimenti ya rasilimali ya maji nchini.

**Maendeleo ya Makazi**

68. Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha 2005-2010 kitaelekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutambua mipaka ya vijiji kwa lengo la kutambua ardhi za vijiji kisheria.

(b) Serikali Kuu kuendelea kuzisaidia serikali za mitaa kupima mipaka ya vijiji katika mikoa ambayo tayari utambuzi wa mipaka umefanyika.

(c) Kuendelea kuimarisha utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.

(d) Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

(e) Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kwa lengo la kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika vya ujenzi wa nyumba bora na kwa gharama nafuu.

(f) Kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

(g) Kulielekeza Shirika la Nyumba la Taifa kuendelea kujenga nyumba za makazi na biashara na kuzifanyia matengenezo nyumba zilizopo.

(h) Kuendeleza miradi ya kupima viwanja katika miji ya makao makuu ya mikoa.

(i) Kujenga mwamko wa kuzingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu katika ujenzi na utengenezaji wa majengo yanayotumiwa na umma.

(j) Kuendelea kuhimiza mashirika yenye mitaji mikubwa kama vile NSSF, PPF na LAPF kujenga nyumba zenye gharama nafuu kwa ajili ya kuwauzia wananchi.

(k) Kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa Serikali kwa ajili ya kuwauzia.

# SURA YA SABA

## MAZINGATIO MAALUMU YA ILANI KUHUSU ZANZIBAR

### Utangulizi

69. Sura hii ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, inatafsiri na kufafanua maeneo muhimu ya sera za CCM kwa kuzingatia mazingira ya Zanzibar. Ushindi wa CCM katika chaguzi kuu za 1995 na 2000 ulitokana na kukubalika kwa siasa na sera zake zinazoweka mbele uhuru, utu, usawa na kutekelezwa kwa misingi ya ukweli na uadilifu.

70. Katika kipindi cha 2000-2005 ambacho ni cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Amani Abeid Karume, mafanikio makubwa yaliweza kupatikana. Kwa kuzingatia sera zake za umoja, amani na mshikamano, CCM ilitiliana saini na CUF Muafaka wa Kisiasa hapo tarehe 10/10/2001 kufuatia mgogoro wa kisiasa uliozuka baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000. Muafaka huo ulijenga mazingira mazuri ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2000. Pia, uliijengea heshima kubwa Zanzibar na Tanzania kwa jumla katika Jumuiya ya kimataifa ambayo ilirejesha imani na misaada kwa Zanzibar iliyokuwa imeizuia toka 1995.

71. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2000 umewezesha kukua kwa uchumi wa Zanzibar kutoka asilimia 4.2 mwaka 2000 hadi asilimia 6.4 mwaka 2004. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini ya asilimia 10 katika kipindi hicho. Aidha, ukusanyaji wa mapato ya Serikali uliongezeka kutoka wastani wa T.sh. 46.7 bilioni kwa mwezi mwaka 2000 hadi T.sh. 64.0 bilioni Juni 2005. Mafanikio hayo yamezaa mafanikio mengi mengine hasa katika kuimarisha huduma za jamii na miundombinu. Kwa mfano, uandikishaji wa watoto wanaofikia umri wa kuanza elimu ya msingi umefikia asilimia 100, na hivyo kuvuka kiwango

cha malengo ya maendeleo ya milenia kuhusu elimu kabla ya mwaka 2015 uliopangwa kimataifa. Katika afya, kiwango cha kutoa chanjo kwa watoto kimefikia asilimia 90. Kwa upande wa miundombinu, zaidi ya kilomita 120 za barabara zilijengwa kwa kiwango cha lami.

72. Mafanikio hayo ya kiuchumi, kijamii na katika maeneo mengine likiwemo la utawala bora yamejenga msingi imara katika mapambano dhidi ya umaskini.

73. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo CCM ikipata ridhaa ya wananchi itaendelea kuiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, (SMZ) katika mwelekeo wa kulinda na kudumisha Mapinduzi ya mwaka 1964 kwa kuendeleza mafanikio yote yaliyopatikana na kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo bado haijakamilika kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuyatambua na kuyaenzi Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964 kuwa ndiyo yaliyoleta uhuru kamili na heshima ya kweli ya Wazanzibari.

(b) Kuendelea kutambua kwamba Mapinduzi hayo sio tu ni ngao ya uhuru wa wananchi wa Zanzibar, bali pia ndio moja ya misingi muhimu ya Muungano wa Tanzania.

(c) Kuendelea kuyalinda na kuyaendeleza kwa nguvu zote mafanikio yaliyoletwa na Mapinduzi hayo, hususan katika sekta ya ardhi, ustawi wa jamii huduma za jamii kama vile elimu na afya, na kukuza uchumi na matumizi endelevu ya rasilimali pamoja na kuwajengea wananchi uwezo wa kutumia fursa zilizopo ili kupambana na umaskini.

(d) Kuendelea kuheshimu haki za binadamu, demokrasia na utawala bora.

74. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2005–2010), CCM itahakikisha kwamba, katika mipango yake ya maendeleo, SMZ

inazingatia kikamilifu **Mwelekeo wa Sera za CCM Katika Miaka ya 2000 hadi 2010, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020** na **Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa ya 2015**. Yote hayo yamezingatiwa katika Ilani hii ya uchaguzi ya CCM.

## Sekta Ya Uchumi

### *Kukuza Uchumi*

75. Katika jitihada za kuendelea kukuza uchumi wa Zanzibar, CCM katika kipindi cha 2005-2010 itaona kwamba SMZ inaendelea kuimarisha utendaji Serikalini, ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuvutia na kulinda vitega uchumi. Hatua zitakazochukuliwa katika kufikia lengo hilo ni pamoja na zifuatazo:-

    (a) Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi na ukusanyaji wa mapato na kupanua wigo wa mapato ya Serikali.

    (b) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mitaji na kuimarisha taasisi na mashirika ya Serikali.

    (c) Kuendeleza mafunzo na kufanya maslahi ya watendaji yawe bora zaidi pamoja na utoaji wa elimu kwa walipa kodi.

    (d) Kusimamia na kuendeleza udhibiti wa matumizi ya fedha na mali za Serikali.

    (e) Kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na kuondosha misamaha isiyo ya lazima.

    (f) Kuendelea kujenga miundombinu itakayoharakisha utekelezaji wa sera ya bandari huru na uwekezaji katika maeneo huru ya kiuchumi ya Fumba, Amani na Micheweni.

(g) Kusimamia utekelezaji wa Sera mpya ya Uwekezaji na Sheria ya Kulinda na Kuhifadhi Vitega Uchumi.

(h) Kukuza na kuendeleza kiwango cha uwekezaji rasilimali na kuimarisha miundombinu ya kisasa.

(i) Kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kukuza mchango wa sekta binafsi katika kuinua uchumi.

## Sekta ya Uchumi

### *Kupambana na Umaskini*

76. Lengo la jitihada za kukuza uchumi wa nchi ni kuimarisha maendeleo na kuinua hali ya maisha ya wananchi. Katika kujiletea maendeleo na kuinua hali zao ni lazima wananchi wenyewe na hasa wale wenye uwezo wa kufanyakazi, washiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma kwa ufanisi na tija. Ili manufaa ya kukua uchumi yawafikie wananchi na kuwawezesha kupambana na umaskini, SMZ chini ya CCM, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Umaskini Zanzibar (**MKUZA**) na kuwaelimisha wananchi na wadau wengine juu ya malengo ya Mpango huo.

(b) Kuendelea kuwaelimisha wananchi hasa wenye uwezo wa kufanyakazi ili washiriki katika shughuli za kujitegemea kwa kutumia juhudi na maarifa ya kisasa (**Modenaizesheni**).

(c) Kuendelea kuitambua rasmi sekta ya kujiajiri hasa katika maeneo ya mijini na kutenga maeneo maalumu ya kufanya shughuli hizo pamoja na kurahisisha taratibu za utoaji leseni.

(d) Kuendelea kuwashirikisha na kuwasaidia wananchi katika juhudi zao za pamoja za kuondoa kero na kujiletea maendeleo katika maeneo yao, hasa katika sekta za ustawi wa jamii kama vile elimu, afya, maji n.k.

## Sekta za Uzalishaji Mali

### *Kilimo*

77. Kilimo ni sekta muhimu kwa uchumi wa Zanzibar na ndio chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi walio wengi hasa wa vijijini. Ili kuongeza tija na mapato ya wakulima, SMZ chini ya CCM itaendelea kuimarisha sekta hii kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera mpya ya Kilimo na kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima kuendesha kilimo cha kisasa kitakachowezesha kutoa mazao mengi katika eneo dogo.

(b) Kuendeleza kilimo cha matunda na viungo kwa kuchanganya na mikarafuu na minazi, likizingatiwa tatizo la ufinyu wa ardhi na haja ya kuongeza aina ya mazao ya biashara.

(c) Kuendeleza na kuimarisha vituo vya huduma za utafiti, elimu kwa wakulima na udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea.

(d) Kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji.

(e) Kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula, biashara na mboga mboga.

(f) Kuwahamasisha na kuwahimiza wazalishaji wa Sekta ya Kilimo kuanzisha vyama vyao vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS).

***Mifugo***

78. Sekta ya Mifugo ni muhimu kwa uchumi wa Zanzibar. Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku wa kisasa, mbali ya kuwapatia wananchi lishe bora pia huongeza kipato na maendeleo yao. SMZ katika kipindi hiki itatilia mkazo na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuwahamasisha na kuwawezesha wafugaji wadogo wadogo kuendeleza ufugaji wa kisasa.

(b) Kuendeleza na kuimarisha vituo vya utafiti, elimu kwa wafugaji na huduma za kinga na tiba, kwa mifugo.

(c) Wafugaji watahamasishwa kumiliki na kuendesha majosho pamoja na maduka ya uuzaji wa madawa ya mifugo.

(d) Kuwahamasisha wawekezaji wa nje na ndani ya nchi ili kuwekeza katika Sekta ya Mifugo na usindikaji wa mazao ya mifugo.

***Uvuvi***

79. Uvuvi ni mojawapo ya shughuli muhimu za kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar. Kutokana na matumizi ya zana duni, wavuvi wengi wanashindwa kuvua katika bahari kuu na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na upungufu wa samaki. Ili kuendeleza uvuvi, SMZ chini ya CCM katika kipindi cha 2005-2010 itatilia mkazo na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo na kutilia mkazo matumizi endelevu ya rasilimali za baharini.

(b) Kuandaa mipango itakayowezesha wavuvi wadogo kupata zana bora za kisasa pamoja na taaluma ya uvuvi bora wenye kujali utunzaji wa mazingira.

(c) Kuihamasisha zaidi sekta binafsi kujiekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kutumia mazingira mazuri ya sheria na vivutio vya uwekezaji.

(d) Kuvutia vitega uchumi katika ujenzi wa kiwanda cha kusindika samaki.

(e) Katika kuliendeleza zao la mwani, wakulima watahamasishwa kuanzisha ushirika wao ili kurahisisha upatikanaji wa nyenzo za uzalishaji na soko la uhakika.

***Maliasili***

80 Visiwa vya Unguja na Pemba vimejaaliwa utajiri mkubwa wa maliasili, ambazo ni vivutio vikubwa kwa watalii. Ili kuendeleza sekta hii, SMZ katika kipindi hiki itaendeleza yafuatayo:-

(a) Hifadhi za mikoko na misitu ya asili, ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Jozani.

(b) Utunzaji wa wanyamapori walio katika hatari ya kupotea kama vile kima punju, popo wa Pemba na paa nunga na kuwatumia kama vivutio vya utalii.

(c) Utunzaji wa viumbehai adimu vya baharini kama vile pomboo na kuvitumia kama vivutio vya utalii.

(d) Kazi za upandaji na uvunaji wa miti, ufugaji wa nyuki na kurina asali.

***Mazingira***

81. Uharibifu wa mazingira ni tishio kwa maendeleo ya Taifa. Matumizi endelevu ya mazingira ni muhimu kwa maslahi ya

kizazi cha sasa na kijacho. Ili kuendeleza hifadhi ya mazingira, SMZ itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia na kuendeleza mpango wa hifadhi ya mazingira katika maeneo ya ardhi, bahari na ukanda wa pwani.

(b) Kuendeleza kazi ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi, ili kuimarisha utunzaji na hifadhi ya mazingira katika maeneo yao.

(c) Kuendeleza kazi ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya makazi, viwanda na mahoteli.

***Utalii***

82. Zanzibar inavyo vivutio vingi vya utalii ukiwemo urithi wa Kimataifa wa Mji Mkongwe wa Zanzibar, fukwe mwanana, misitu ya asili, wanyama, magofu n.k. Ili kuendeleza Sekta ya Utalii na kukuza Pato la Taifa, SMZ chini ya CCM itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Kuendeleza Shughuli za Utalii (*Tourism Master Plan*) na kuendelea kuitangaza Zanzibar kwa lengo la kutafuta masoko mapya ya utalii, mfano China na nchi nyingine za Mashariki ya mbali.

(b) Kuweka taratibu zitakazopunguza mianya ya uvujaji wa mapato kupitia "*package tourism*", bila ya kuathiri soko.

(c) Kuimarisha miundo mbinu yenye kuendeleza Sekta ya Utalii na kutilia mkazo utalii wa daraja la kwanza, wenye kuzingatia mila, desturi na utamaduni wa Mzanzibari. Miundombinu hiyo ni pamoja na hoteli za hadhi ya juu za nyota 3 hadi 5.

(d) Kuimarisha mafunzo katika fani zote za utalii kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma kwa watalii.

(e) Kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii, katika maeneo yanayoendesha biashara ya utalii.

(f) Kuvutia wawekezaji makini wenye uwezo katika Sekta ya Utalii, hususan katika hoteli zitakazoingia kwenye mitandao ya hoteli za hadhi ya juu kimataifa kama vile Sheraton , Hilton na Intercontinental.

***Biashara na Viwanda***

83. Kwa kuzingatia kwamba Zanzibar ni visiwa na inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa ardhi, shughuli kubwa kiuchumi zinahitaji kuelekezwa kwenye viwanda na biashara. Kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza shughuli hizo katika kipindi cha 2005-2010, SMZ chini ya CCM itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Mpango na Sera ya Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo na Viwanda vya Kati.

(b) Kuwaendeleza wazalishaji wadogo wadogo na kuimarisha fursa za kuanzisha viwanda vitakavyotumia malighafi inayopatikana nchini.

(c) Kuendeleza kazi ya utafutaji wa masoko mapya kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar, na kudhibiti ubora wa bidhaa hizo na zile zinazoingizwa nchini.

(d) Kuendeleza jitihada za kuanzisha viwanda vinavyozalisha ajira nyingi, kama vile vya nguo, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sekta binafsi.

(e) Kukamilisha maandalizi ya Sera mpya ya Biashara na kufanya marekebisho ya sheria za biashara.

(f) Kuendeleza mazungumzo na nchi mbali mbali ili kukuza mashirikiano na kupanua wigo wa masoko ya nje.

(g) Kuandaa mpango wa kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo wadogo.

(h) Kuanzisha Baraza la Biashara ambalo litakuwa na wajumbe kutoka Serikalini na sekta binafsi.

(i) Kuwezesha uzalishaji katika maeneo huru ya kiuchumi kwa ajili ya masoko ya Marekani (AGOA), Ulaya (EBA) na mengineyo.

(j) Kuongeza harakati za biashara ya kimataifa katika eneo la Bandari Huru la Maruhubi.

***Ushirika***

84. CCM inatambua umuhimu wa Ushirika kama mkombozi wa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara wadogo wadogo. Aidha, ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS) ni muhimu sana kwa kusaidia wananchi kupata chanzo cha mitaji. Ili kuimarisha na kuendeleza sekta hii, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa programu maalum ya uimarishaji wa Sekta ya Ushirika iliyoandaliwa kipindi kilichopita.

(b) Kuendeleza kazi ya ukaguzi na utoaji wa mafunzo na mbinu za uzalishaji, utunzaji wa rasilimali na uendeshaji wa vyama vya ushirika.

(c) Kuendelea kuwahamasisha wananchi kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS).

## Sekta za Miundombinu ya Kiuchumi

85. Maendeleo endelevu ya kiuchumi ni lazima yaendane na hatua thabiti za uimarishaji wa miundombinu ya kiuchumi, ambayo hujumuisha huduma za mawasiliano ya barabara, bandari, usafiri wa baharini, usafiri wa anga, umeme n.k. Ili kuimarisha zaidi miundombinu ya kiuchumi, CCM itahakikisha kuwa, hatua zifuatazo zinatekelezwa:-

### *Barabara*

86. Barabara kuu na za vijijini ni miundombinu ya msingi katika harakati za kiuchumi za wananchi kama vile kuyafikia kwa urahisi masoko ya mazao yao. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itahimiza SMZ kufanya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha kazi ya ujenzi wa barabara ya Jang'ombe – Mpendae (Km 1.2).

(b) Kujenga jumla ya Km 156 za barabara za Unguja na Km 105 za barabara za Pemba, kama ifuatavyo:-

*Unguja*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1) Mazizini | - | Fumba | Km 17.81 |
| 2) Mfenesini | - | Bumbwini | Km 13 |
| 3) Welezo | - | Dunga | Km 12.75 |
| 4) Tunguu | - | Kinyasini | Km 26.77 |
| 5) Makunduchi | - | Jambiani/Paje | Km 17 |
| 6) Mkwajuni | - | Nungwi | Km 18.8 |
| 7) Pongwe | - | Matemwe | Km 20.4 |
| 8) Paje | - | Pingwe | Km 16.8 |
| 9) Donge | - | Mkokotoni | Km 12.8 |

*Pemba*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1) | Kengeja | - | Mtambile | Km 6.6 |
| 2) | Kenya | - | Chambani | Km 3.2 |
| 3) | Mizingani | - | Wambaa | Km 10 |
| 4) | Tundaua | - | Pujini | Km 15 |
| 5) | Mtambile | - | Kangani | Km 6.2 |
| 6) | Chake | - | Wete | Km 30 |
| 7) | Wete | - | Konde | Km 15 |
| 8) | Wete | - | Gando | Km 13 |
| 9) | Mkoani | - | Makombeni | Km 6 |

(c) Kuendeleza kazi ya matengenezo na utunzaji wa barabara kuu, barabara za mijini na vijijini.

## *Bandari*

87. Kwa kuzingatia kwamba uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa visiwa, bandari ina umuhimu wa pekee. Katika kipindi cha 2005-2010, SMZ chini ya CCM itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Mpango Mkuu (*Master Plan*) wa Bandari ya Malindi ikijumuisha huduma za bandari huru, na kusimamia utekelezaji wake.

(b) Kuifanyia matengenezo makubwa Bandari ya Malindi, likiwemo eneo maalum la kuwekea makontena na kutenganisha eneo la huduma za mizigo na abiria pamoja na kuipatia vifaa vya kisasa.

(c) Kuimarisha na kuiendeleza gati ya Wete kwa kuongeza urefu wa ngazi yake kutoka mita 114 za sasa hadi mita 125 na upana wa mita 6.

(d) Kuendelea kuitengeneza Bandari ya Mkoani kuwa ni Mlango Mkuu (*Entry Point*) wa kuingilia meli na kuifanyia matengenezo yanayohitajika.

(e) Kuimarisha gati ya Mkokotoni kwa kujenga jeti kwa ajili ya majahazi na usafiri wa wananchi hasa wa Tumbatu.

(f) Kuanzisha ujenzi wa gati ya Wesha, Pemba.

***Usafiri wa Baharini***

88. Katika kuendelea kuimarisha huduma za usafiri wa baharini, CCM katika kipindi cha 2005-2010 itaona kwamba SMZ inachukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(a) Kuendeleza kazi ya kujenga mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani, kuwekeza zaidi katika sekta ya usafiri wa baharini.

(b) Kuendeleza jitihada za kuliimarisha Shirika la Meli la Zanzibar ili lijiendeshe kibiashara na kuwavutia wawekezaji binafsi kuingia ubia.

***Usafiri wa Anga***

89. Katika jitihada za kukuza utalii, usafiri wa anga ni lazima uwe wa ubora unaokubalika kimataifa. Katika kipindi cha 2005-2010 SMZ chini ya CCM itaendeleza hatua zilizoanza kuchukuliwa kipindi kilichopita zikiwemo zifuatazo:-

(a) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar.

(b) Kuendeleza na kukamilisha kazi ya matengenezo ya jengo la Kiwanja cha Ndege cha Karume – Pemba.

(c) Kuendeleza kazi ya kuimarisha huduma za Usalama wa abiria na mizigo na kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa, wafanyakazi wa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar na Karume – Pemba.

(d) Kujenga jengo jipya la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar.

### *Umeme*

90. Upatikanaji wa umeme ni muhimu katika kuwezesha uzalishaji viwandani na kuyafanya maisha ya wananchi mijini na vijijini kuwa bora. CCM katika kipindi cha 2005-2010 itaona kwamba SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza mipango ya usambazaji wa huduma ya umeme kwa wananchi mijini na vijijini.

(b) Kuendeleza juhudi za kupatikana kwa chanzo mbadala cha umeme Kisiwani Pemba pamoja na kuimarisha vinu vilivyopo hivi sasa.

(c) Kuandaa mipango na mikakati ya kuwavutia wawekezaji, ili kuwekeza na kuzalisha umeme kwa njia nyingine.

### *Ardhi*

91. Ardhi ni mojawapo ya rasilimali na nguzo kuu katika ujenzi wa uchumi. Maendeleo ya nchi yetu katika sekta mbali mbali yanategemea sana rasilimali hii. CCM katika kipindi hiki itahakikisha kuwa:-

(a) Ardhi inaendelea kuwa ni mali ya Serikali kwa faida na maslahi ya wananchi wote.

(b) Wananchi wanaelimishwa juu ya umuhimu wa kuzingatia matumizi bora na endelevu ya ardhi na Serikali inaendeleza udhibiti wake kwa mujibu wa sheria zilizopo na zitakazowekwa.

(c) Kuendeleza kazi ya upimaji, uthamini, usajili na utoaji wa hati za umilikaji wa ardhi, ili kuwawezesha wananchi

kutumia ardhi wanayoimiliki kama dhamana ya maendeleo yao.

(d) Kuendeleza utekelezaji wa mpango wa Kitaifa wa matumizi bora ya ardhi, hususani kuyatenga maeneo yenye rutuba kwa ajili ya matumizi ya kilimo.

(e) Kukamilisha utayarishaji wa ramani mpya za Visiwa vya Unguja na Pemba.

## Sekta za Huduma za Jamii

### *Elimu*

92. CCM inatambua kwamba, elimu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi na ndio ufunguo wa maendeleo. Ili uendeleza sekta hii hatua zifuatazo, zitatekelezwa:-

(a) Kuendeleza juhudi za kupanua elimu ya awali.

(b) Kuhakikisha kuwa, kazi ya uandikishaji inaendelezwa na watoto wenye umri wa kuanza elimu ya msingi wanapatiwa nafasi za masomo. Aidha, watoto wenye ulemavu, watapatiwa nafasi ya kusoma katika skuli zilizo karibu na maeneo yao na kufundishwa katika madarasa ya kawaida.

( c) Kupanua elimu ya sekondari katika ngazi za Kidato cha I-IV na V-VI

(d) Kuimarisha mafunzo ya ualimu.

(e) Kuanzisha vituo vya kazi za amali na elimu mbadala na kuimarisha mazingira ya skuli za Serikali na binafsi, ili kuibua vipaji vipya vya wahitimu kwa kuzingatia mahitaji ya soko na kuwajengea uwezo wa kujiajiri wao wenyewe.

(f) Kukamilisha ujenzi wa Maktaba Kuu.

(g) Kuendeleza mipango ya kuwashirikisha wananchi wenyewe katika kuinua kiwango cha elimu na kuchangia gharama za utoaji wa huduma za elimu.

(h) Kuzingatia ipasavyo suala la ubora wa elimu, kama linavyoshughulikiwa suala la wingi.

(i) Kuendeleza na kuimarisha fursa za elimu ya juu, sayansi na teknolojia kwa kuvipanua vyuo vikuu vilivyopo na kutazama uwezekano wa kuanzisha vipya.

(j) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu iliyoandaliwa na kuendeleza maslahi ya walimu.

(k) Kuendeleza kazi ya kuwahamasisha wananchi kujiunga na kisomo chenye manufaa ili kuondokana na ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

(l) Kuhakikisha kuwa, elimu ya watu wazima inayotolewa inawapatia walengwa ujuzi utakaowawezesha kupambana na umaskini.

(m) Kuendeleza elimu ya sayansi kwa wasichana.

***Afya***

93. Afya bora kwa wananchi wote ni miongoni mwa malengo muhimu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964. Aidha, sekta hii imepewa kipaumbele katika Mpango wa Kupunguza Umaskini. Ili kuendeleza huduma za afya kwa wananchi mijini na vijijini, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya na ushirikishwaji wa wananchi katika kuchangia maendeleo na kuimarisha kiwango cha huduma za afya.

(b) Kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi ili kujikinga na aina mbali mbali za maradhi ya kuambukiza.

(c) Kuimarisha huduma za Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili kufikia hadhi na kiwango cha Hospitali ya Rufaa. Aidha, kiwango cha huduma za hospitali na vituo vingine vya afya zitaimarishwa.

(d) Kuimarisha huduma za utafiti na udhibiti wa maradhi ya kuambukiza, uzazi salama na hifadhi ya mama na mtoto.

(e) Kujenga na kuanzisha kituo cha waathirika wa dawa za kulevya.

(f) Kuendeleza mafunzo na kuinua kiwango cha maslahi ya watendaji wa Sekta ya Afya.

(g) Kuzidisha mapambano dhidi ya UKIMWI kwa njia za kuwaelimisha wananchi, kuwahimiza kupima afya zao, matumizi ya dawa za kupunguza maambukizo ya mama kwa mtoto na zile za kurefusha maisha kwa waathirika na kuimarisha huduma za uchunguzi.

(h) Kuimarisha na kuendeleza vituo vya ushauri nasaha, huduma za tiba kwa waathirika na kupiga vita unyanyapaa.

***Maji***

94. Maji ni miongoni mwa huduma muhimu kwa wananchi wote. Ili kuendeleza juhudi za usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa sera ya taifa ya maji pamoja na sheria zinazohusika.

(b) Kuendeleza utekelezaji wa malengo na miradi ya maji, ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata huduma ya maji safi na salama.

(c) Kuendeleza na kuimarisha utaratibu wa kuwashirikisha wananchi wenyewe mijini na vijijini katika kuchangia gharama za utunzaji na uendeshaji wa mitambo pamoja na hifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji.

***Makazi***

95. Moja ya malengo muhimu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964, ni kuwapatia wananchi nyumba bora za kuishi mijini na vijijini. Ili kuendeleza azma hiyo, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Nyumba na kusimamia utekelezaji wake.

(b) Kukamilisha kazi ya ujenzi wa nyumba za maendeleo kama vile za Michenzani na kuandaa mipango ya kuzigawa kwa wale wanaostahili.

(c) Kuendeleza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba bora na kuwahamasisha wananchi kujijengea nyumba za kuishi.

(d) Kuandaa mpango na taratibu za kuwashirikisha wananchi wanaoishi katika nyumba za maendeleo mijini na vijijini, kuchangia gharama za matengenezo na utunzaji wa nyumba hizo.

(e) Kuanzisha sera ya kujenga nyumba za ghorofa kwa kuzingatia ufinyu wa ardhi.

## Maeneo Mengine Ya Kipaumbele

### *Utamaduni na Michezo*

96. Kudumisha utamaduni na kuendeleza michezo ni masuala yenye umuhimu mkubwa kwa uhai na maendeleo ya Taifa. Aidha, michezo na sanaa hutoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuwaunganisha wananchi. Ili kuendeleza sekta hii CCM itahakikisha kuwa hatua zifuatazo zinatekelezwa:-

    (a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Utamaduni na Sera ya Michezo na kusimamia utekelezaji wake.

    (b) Kuendelea kuhimiza na kusisitiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbali mbali ya maendeleo.

    (c) Kuvitambua, kuvikuza na kuviendeleza vipaji vya wanamichezo na wasanii kwa kuunda timu za michezo na sanaa za aina mbali mbali katika ngazi za Vijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa.

### *Vyombo vya Habari*

97. CCM inatambua na kuthamini sana mchango wa vyombo vya habari katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuimarisha demokrasia. Ili kuimarisha sekta hii hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

    (a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Habari na kusimamia utekelezaji wake.

    (b) Kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na kuingiza teknolojia ya kisasa ya mawasiliano ya habari.

    (c) Kuendeleza kazi ya kuimarisha studio za TVZ na STZ kwa kuzipatia vifaa vya kisasa, matengenezo ya majengo na mafunzo kwa watendaji.

(d) Kuimarisha utendaji wa Tume ya Utangazaji, kusimamia haki na wajibu wa vyombo vya habari pamoja na maadili ya waandishi wa habari.

(e) Kuimarisha mafunzo ya uandishi wa habari yanayotolewa na Idara ya Habari (Maelezo).

### *Majanga Na Huduma za Uokoaji*

98. Ili kuimarisha huduma za uokoaji na mbinu za kukabiliana na majanga ya aina mbali mbali, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(a) Kikosi cha Zima Moto na Uokoaji (KZU) kitaimarishwa zaidi kwa kupatiwa mafunzo na vifaa vya kisasa.

(b) Elimu itatolewa kwa wananchi ili kujenga uwezo wao katika kukabiliana na kujikinga na majanga mbali mbali.

(c) Kuimarisha huduma za zimamoto katika viwanja vya Ndege vya Zanzibar na Karume, Pemba. Aidha, vituo vya zimamoto na uokoaji vitaanzishwa na kuimarishwa katika kila Mkoa.

### *Demokrasia na Utawala Bora*

99. CCM ni muumini thabiti wa dhana za demokrasia na utawala bora ambazo misingi yake ni madaraka ya wananchi, utawala wa sheria uwajibikaji na uadilifu (vita dhidi ya rushwa). Katika kuzidi kuimarisha misingi ya demokrasia na utawala bora katika kipindi cha 2005-2010, CCM itahakikisha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(a) Kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya nchi, Kanuni na taratibu zilizowekwa kidemokrasia.

(b) Kukamilisha maandalizi ya sera na sheria ya utekelezaji wa Mpango wa Utawala Bora na kusimamia utekelezaji wake.

(c) Kuendeleza utoaji wa mafunzo na mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Utawala Bora kwa Viongozi na Watendaji wa ngazi mbali mbali za Serikali na wananchi.

(d) Kusimamia utekelezaji wa haki za binaadamu kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar, na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tamko la Haki za Binaadamu la Umoja wa Afrika na la Umoja wa Mataifa.

(e) Kuhakikisha kuwa, demokrasia ya kweli inapewa kipaumbele na kutekelezwa katika ngazi zote za maamuzi.

(f) Kuendeleza mafunzo na elimu ya demokrasia kwa wananchi, ili kukuza uelewa wao na kujenga mahusiano mazuri kati yao na Serikali.

(g) Kuweka na kusimamia utaratibu mzuri zaidi wa kupokea kero za wananchi na kuhakikisha kuwa zinapatiwa ufumbuzi wa haraka.

(h) Kuhakikisha kuwa, Vyama vya Siasa vinaheshimu demokrasia ya kweli na kufuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na zitakazowekwa.

(i) Kuandaa mpango na mkakati wa ujenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi lenye hadhi na heshima mbele ya jamii.

(j) Kukamilisha maandalizi ya Sera mpya ya Serikali za Mitaa na kusimamia utekelezaji wake.

(k) Kuhakikisha kuwa Serikali Kuu, inaendelea kuziwezesha na kuzisaidia Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(l) Kuwaelimisha na kuwaongoza wananchi katika mtazamo wa kuzitumia Serikali za Mitaa kama nyenzo katika kujiletea maendeleo na kupambana na umaskini.

(m) Kuendeleza mafunzo ya sheria na uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa watendaji na Madiwani wa Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa.

(n) Kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinabuni mbinu na mikakati muafaka ya kupambana na tatizo sugu la wizi wa mifugo na mazao ya wakulima katika maeneo yao.

(o) Kuhakikisha kuwa, viongozi wa kuchaguliwa wanaendelea kupatikana kwa ridhaa ya wananchi.

(p) Kuendeleza na kuimarisha mazingira yenye kuthibitisha kwamba, wananchi ndio wenye madaraka ya kuongoza Serikali, na kwamba wanashirikishwa kikamilifu katika kupanga na kusimamia maendeleo yao.

(q) Kuhakikisha kuwa, Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa zinawajibika kwa wananchi na kuunga mkono juhudi zao za kupambana na umaskini.

(r) Kuimarisha **mapambano dhidi ya rushwa** na kutunga Sheria ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi. Taasisi maalum ya kusimamia na kuchunguza tuhuma za rushwa itaanzishwa.

(s) Kuendeleza mafunzo na elimu kwa wananchi kuhusu rushwa. Aidha, vikundi vya kijamii vitahamasishwa kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa.

### *Ulinzi na Usalama*

100. Kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Vikosi Maalum vya SMZ vitaendelezwa kwa kupatiwa mafunzo, nyenzo na zana za kisasa.

(b) Kuendeleza na kuimarisha mashirikiano mema kati ya Vikosi Maalum vya SMZ na Vyombo vya Ulinzi na Usalama hususan katika mafunzo na ulinzi wa raia na mali zao.

(c) Wananchi na hasa vijana wataendelea kuhamasishwa ili kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao wanayoishi.

***Kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar***

101. Sera ya kuwaunganisha na kuwashirikisha wananchi wa Zanzibar katika harakati za ujenzi wa Taifa lao kwa amani na utulivu, zilipewa umuhimu mkubwa katika kipindi kilichopita. Kufikiwa kwa Muafaka wa kisiasa tarehe 10 Oktoba 2001, kati ya CCM na CUF ni uthibitisho tosha wa usahihi wa Sera za CCM. Ili kuimarisha mafanikio hayo ya kujivunia, CCM katika kipindi hiki itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza matunda ya Muafaka kwa faida na maslahi ya Wazanzibari wote.

(b) Kuendelea kupiga vita kwa nguvu zote ubaguzi wa dini, kabila, jinsia au asili ya mtu katika utoaji wa huduma na fursa mbali mbali za kiuchumi na kijamii.

(c) Kuendeleza umoja, mshikamano, amani na utulivu miongoni mwa wananchi wote na kuimarisha jumuiya mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali**

***Watoto***

102. Chama cha Mapinduzi kinatambua na kuthamini sana umuhimu wa mtoto kupewa haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa na

kutobaguliwa kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya nchi. Ili kuendeleza na kuimarisha haki na Maendeleo ya mtoto, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali na vituo vyote vya afya na kuhakikisha kuwa watoto wote wanapatiwa Kinga za magonjwa mbali mbali katika muda unaofaa.

(b) Kuendeleza mapambano dhidi ya ajira za watoto na kusimamia utekelezaji wa Sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu haki na usawa wa mtoto.

(c) Kusimamia na kuratibu ubora wa mashirika ya hiari na watu mbali mbali wanaoshughulikia vituo vya kulishia na kulelea watoto pamoja na Skuli za awali.

***Vijana***

103. Vijana ni kundi lenye nguvu na uwezo mkubwa wa kufanya kazi na kuendeleza jamii. Ili kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili vijana na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Kuviendeleza vikundi vya vijana na kuwahamasisha ili kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

(b) Kuimarisha na kuendeleza elimu ya amali na mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri wenyewe na kujitegemea.

(c) Kuhamasisha taasisi za fedha ili kuwapatia vijana mikopo ya masharti nafuu.

(d) Kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi, upatikanaji wa ajira kwa vijana wazalendo na kusimamia haki na mazingira bora ya kazi.

(e) Kuendeleza vita dhidi ya dawa za kulevya, ili kuwakinga vijana wasiathirike na dawa hizo pamoja na UKIMWI.

***Wanawake***

104. Kwa kutambua na kuthamini nafasi na mchango wa wanawake katika maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, CCM itahakikisha kwamba hatua zifuatazo zinatekelezwa:-

(a) Kuendelea kupiga vita mila, desturi na sheria zinazowabagua wanawake pamoja na kusimamia sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa wanawake.

(b) Kuhamasisha na kushajiisha juu ya kuwepo na fursa sawa bila kujali jinsia katika elimu, nafasi za uongozi, na utawala.

(c) Kuhamasisha taasisi za fedha ili kuwawezesha wanawake kiuchumi.

***Wazee***

105. Kwa kutambua umuhimu wa wazee na mchango wao katika ujenzi wa taifa letu, CCM itahakikisha kuwa, hatua zifuatazo zinatekelezwa:-

(a) Kuhakikisha kuwa wazee wasiojiweza wanaendelea kupatiwa hifadhi ya makazi, huduma za afya na msaada wa kijamii.

(b) Kuhakikisha kuwa maandalizi madhubuti yanakuwepo kabla ya mfanyakazi kustaafu na kwamba utaratibu unawekwa wa kuwa na kima cha chini cha malipo ya pensheni kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na hali ya maisha.

(c) Wazee kuendelea kupewa nafasi wanayostahili na kutambulika kuwa ni rasilimali yenye thamani kubwa katika jamii.

## *Walemavu*

106. Kwa kuzingatia kwamba binadamu wote ni sawa, CCM itaendelea kuelimisha jamii ili kuondokana na fikra potofu juu ya ulemavu na walemavu. Aidha, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(a) Kuendelea kuwapatia huduma za msingi watu wenye ulemavu na kuwashirikisha katika shughuli za utendaji na uongozi.

(b) Kuendeleza na kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ufundi kwa watu wenye ulemavu na kuwapatia vitendea kazi na fursa za mikopo ili waweze kujiajiri na kujitegemea.

(c) Kuendelea kulinda na kusimamia haki, usawa na maendeleo ya watu wenye ulemavu, kwa mujibu wa Katiba, Sera na Sheria za nchi.

# SURA YA NANE

## MAENEO MENGINE MUHIMU

### Demokrasia na Utawala Bora

#### *Utawala Bora*

107. Hatua mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kuimarisha utawala bora nchini katika kipindi cha Awamu ya Tatu. Katika kipindi hiki cha 2005-2010 CCM itazielekeza Serikali kuendeleza utawala bora kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa kidemokrasia nchini kote kuanzia ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa.

(b) Kuendelea kutoa mafunzo juu ya utawala bora kwa watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo hayo yanaiweka Serikali kwenye utendaji ulio wazi.

(c) Kuzingatia kwa ukamilifu haki za binadamu katika utendaji wa vyombo vya dola.

(d) Kuliimarisha Jeshi la Polisi kwa kuliongezea uwezo wa taaluma na zana za upelelezi ili upelelezi wa kesi uwe ukikamilika haraka na hivyo kupunguza kero ya mahabusu kukaa muda mrefu magerezani.

(e) Kuendelea kupunguza msongamano magerezani.

## *Sekta ya Sheria*

108. CCM itazitaka Serikali ziendelee na hatua zilizoanza kuchukuliwa ili kuiboresha Sekta ya Sheria kusudi nayo itoe huduma bora zaidi kwa jamii. Yatakayosisitizwa katika kipindi hiki ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuzifanyia marekebisho sheria za mirathi na zile zinazoonekana kuwakandamiza wanawake.

(b) Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara.

(c) Kuanzisha na kutekeleza mpango maalumu wa kuanzisha Ofisi za Mahakama Kuu katika kila Mkoa.

(d) Kukamilisha mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashitaka.

(e) Kuziimarisha na kuzioanisha sheria zinazohusiana na mapambano dhidi ya rushwa.

(f) Kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hususani ujenzi wa majengo ya mahakama ya ngazi zote na kuajiri majaji na mahakimu wa kutosha.

(i) Kuweka mfumo wa kuwasaidia wananchi wasiojiweza kupata msaada wa kisheria.

(j) Kuweka mfumo utakaowezesha kutumika kwa wanasheria wa awali (*para-legals*) katika mahakama za mwanzo.

## *Demokrasia na Madaraka ya Umma*

109. Katika jitihada za kukuza demokrasia na kuimarisha madaraka ya wananchi, CCM itaona kwamba Serikali zinahimiza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha na kutoa elimu ya demokrasia katika ngazi zote na kujenga uvumilivu wa kisiasa nchini.

(b) Kuendelea kuimarisha mfumo wa **demokrasia ya kibunge** (*parliamentary democracy*) hadi katika ngazi ya halmashauri.

(c) Kujenga utamaduni unaoheshimu haki ya wananchi kujadili na kuhoji mambo yanayohusu nchi yao na kuheshimu dhamana na haki ya vyombo halali ya kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa kihalali ili shughuli za nchi ziendelee.

(d) Kwamba vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu na pia vyama halali visivyo vya kiserikali vinapewa nafasi ya kuendesha shughuli zao kama ilivyokusudiwa na sheria.

(e) Kuendeleza mahusiano mazuri kati ya wananchi na Serikali zao kwa kutumia uongozi shirikishi katika kushughulikia masuala yao.

(f) Kuvihimiza vyama vyote vya siasa kujenga na kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vyao.

(g) Kwamba vyama vya siasa vinakubaliana juu ya maadili yatakayoongoza shughuli zao miongoni mwa wananchi na kuongoza uhusiano kati ya vyama vyenyewe

(h) Kuhakikisha utaratibu uliopo wa wananchi kuchagua viongozi wao kwa misingi ya demokrasia unadumishwa;

(i) Kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa katika kupanga na kusimamia maendeleo yao;

(j) Kuendelea kuhimiza serikali za mitaa ziunge mkono juhudi za wananchi za kupambana na umaskini;

(k) Kuhakikisha kuwa serikali za mitaa zinakuwa na mipango mizuri itakayoziongezea mapato yatakayosaidia kutoa huduma bora za jamii.

### *Mapambano Dhidi ya Rushwa*

110. Serikali ya Awamu ya Tatu imeleta mafanikio makubwa katika vita dhidi ya rushwa. Matokeo mazuri ni pamoja na ongezeko kubwa la mapato ya Serikali kutokana na kuzibwa kwa mianya ya rushwa. Vile vile maafisa wengi wameshitakiwa na wengine kadha kuachishwa kazi n.k. Katika kipindi cha 2005-2010 CCM na Serikali zitaongeza jitihada za:-

(a) Kuendelea kuchukua hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa.

(b) Kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari, na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma.

(c) Kufuatilia malalamiko ya baadhi ya wananchi kwamba kuna watu wengi wanaolimbikiza mali nyingi kama majumba, mashamba n.k. kuliko uwezo wa mapato halali wanayoyapata.

(d) Kuendelea kuziba mianya ya rushwa katika utendaji wa Serikali.

(e) Kushughulikia kwa nguvu zaidi malalamiko ya wananchi ya kero ya rushwa ndani ya vyombo vya dola kama vile Polisi na vyombo vya huduma za jamii kama hospitali, shule na mahakama.

(f) Katika mafunzo ya elimu ya uraia, wananchi watachochewa kuichukia rushwa katika siasa na kuwadharau viongozi watoa na wapokea rushwa.

## Ulinzi na Usalama

111. Katika kipindi cha 2005-2010 Serikali za CCM zitaendelea na utekelezaji wa majukumu yafuatayo kwenye sekta hii:-

(a) Kuendeleza sera ya CCM ya kuwa na majeshi madogo ya ulinzi wa nchi na usalama wa raia yenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa.

(b) Kuwahamasisha wananchi ili waendelee kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao na kuhakikisha usalama wao na wa mali zao. Utaratibu wa **Polisi Jamii** utawekwa kwa ajili ya kuwa na mfumo mzuri zaidi wa kushirikisha vikundi vya ulinzi wa jadi na makampuni binafsi ya ulinzi.

(c) Kuvijengea mazingira mazuri vyombo vya ulinzi na usalama na kuendelea kutatua matatizo ya makazi na maslahi ya watumishi wake.

(d) Kuongeza uwezo wa Taifa wa kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo.

(e) Kuandaa upya Sera ya Uhamiaji itakayobainisha masuala ya uraia na ukaazi katika mazingira mapya ya kuelekea ushirikiano katika SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(f) Kuanzisha na kutoa vitambulisho vya uraia.

(g) Kuongeza kasi ya urejeshaji wa wakimbizi makwao kadiri hali inavyoruhusu; na pia kuihimiza Jumuiya ya Kimataifa kusaidia uhuishaji wa mazingira na miundombinu iliyoharibiwa na kuwepo kwa wakimbizi;

(h) Kuendeleza ufufuaji wa JKT uliokwisha kuanza na kuutafakari kwa undani muundo mpya unaolingana na hali ya sasa ili kutekeleza malengo ya awali ya kulinda na kujenga nchi, kuimarisha umoja wa kitaifa na kuwajenga vijana katika uzalendo wa hali ya juu..

**Hifadhi ya Mazingira**

112. Katika kipindi cha 2005-2010, Serikali za Chama Cha Mapinduzi zitajielekeza kufanya yafutayo katika kuhakikisha kazi iliyoanza ya hifadhi ya mazingira inakuwa endelevu:-

(a) Kuendeleza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa wao kuhusu hifadhi ya mazingira.

(b) Kuhamasisha na kuwezesha utumiaji wa matanuri ya kisasa ya kuchomea mkaa yenye sifa ya kupunguza upotevu wa miti.

(c) Kutazama uwezekano wa kutumia makaa ya mawe kwa kupikia.

(d) Kuhamasisha matumizi ya majiko yenye kutumia mkaa/kuni kidogo.

(a) Kujenga mwamko katika jamii wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya hali ya hewa nchini (*climate change*).

(b) Kuendeleza kampeni ya upandaji miti ambayo imekuwa ikifanywa kila mwaka na kuhakikisha kwamba miti inayopandwa inatunzwa ipasavyo, na kuhimiza tabia ya kutokukata miti ovyo.

(c) Kutoa elimu kuhusu sheria ya mazingira kwa wananchi.

(d) Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka ngumu ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

(e) Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vitakavyotumia taka ngumu kama mali ghafi.

## Kujenga Uwezo wa Kukabili Majanga

113. Majanga ni matukio yenye asili ya maumbile au ya binadamu wenyewe ambayo husababisha athari kubwa kwa binadamu, mali na mazingira. Majanga makubwa ni pamoja na tsunami, tetemeko la ardhi, mvua za kimbunga, myoto mikubwa, n.k. Matukio ya mvua za *El Nino* na ajali ya M.V. Bukoba yametuonyesha umuhimu wa nchi kujiandaa kwa zana na maarifa ya uokoaji.

114. Katika miaka mitano ya Ilani hii, CCM itazielekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga ya moto.

(b) Kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na dharura za ajali za halaiki katika maeneo nyeti na ya watu wengi k.v. Red Cross, hospitali, vyombo vya dola, n.k.

(c) Kujenga uwezo wa vyombo vya dola wa kudhibiti na kukabiliana na majanga ya kimaumbile kama tsunami, tetemeko la ardhi, tufani na mvua za kimbunga, mafuriko na ukame mkubwa.

(d) Kuitazama upya Idara ya Maafa ya Serikali kwa lengo la kupata njia za kuiimarisha.

## Utafiti na Maendeleo

115. Tume ya Sayansi na Teknolojia ilianzishwa kwa madhumuni ya kuipa sayansi na teknolojia **nafasi ya kati** katika maendeleo ya nchi yetu. Ilikusudiwa pia kuongoza na kuratibu shughuli za utafiti na maendeleo zinazofanywa na taasisi mbalimbali bila uratibu. Kutokana na umuhimu wa utafiti katika sayansi na

teknolojia, CCM itazitaka Serikali kuweka mbele hatua zifuatazo:-

(a) Utafiti na Maendeleo (*Research and Development* – R& D) pamoja na shughuli za Tume ya Sayansi na Teknolojia kutengewa kiasi cha angalau asilimia l.0 ya Bajeti ya Serikali kila mwaka.

(b) Kuingia katika utaratibu wa kusajili na kulinda ("*patenting*") hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti wenyewe na kwa Taifa.

(c) Kuhamasisha na kuhimiza uzalishaji kibiashara wa zana(prototype) zinazotokana na tafiti mbali mbali ili ziweze kusambazwa kwa watumiaji. Aidha, kwa upande wa kilimo, kuanza uzalishaji kibiashara nchini wa mbegu bora zilizotafitiwa na kuzisambaza kwa wakulima.

(d) Kuliingiza Shirika la **Nyumbu** katika mkondo wa taasisi za utafiti, pamoja na kuhimiza fani yake ya uundaji wa magari kibiashara.

## Vyombo vya Habari

116. Kwa kuzingatia mchango mkubwa unaotolewa na vyombo vya habari katika jamii, katika kipindi cha 2005–2010 CCM itazitaka Serikali zichukue hatua zifuatazo:-

(a) Kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari kwa mujibu wa sheria.

(b) Kueneza Radio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa (TVT) nchi nzima na kuwa hewani kwa saa 24 kila siku.

(c) Kuanzisha gazeti la Kiswahili la Serikali.

(d) Kuinua ubora wa taaluma ya habari kwa kushirikiana na wamiliki wa vyombo vya habari vya binafsi.

(e) Kwa kushirikiana na vyombo vyao vya uwakilishi, kuweka mipango ya kuwaelimisha waandishi wenye vipa ji katika taaluma maalum ili tuanze kuwapata waandishi wanaoweza kuyasanifu na kuyachambua masuala ya uchumi, siasa, ulinzi n.k. katika vyombo mbali mbali.

## Mambo ya Nje

117. Mwelekeo wa sasa wa Sera ya CCM ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, unaongozwa na **Sera ya Diplomasia ya Uchumi,** hivyo ofisi zetu za Ubalozi zinahitaji ziimarishwe kiutalaamu. Katika kipindi cha 2005–2010, msisitizo utakuwa katika kuendeleza Displomasia ya Uchumi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa na watalii.

(b) Kuendeleza sera ya ujirani mwema na nchi jirani.

(c) Kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Jumuiya ya Uchumi Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Afrika (AU), Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote na Umoja wa Mataifa.

(d) Kulitangaza jina la nchi yetu na kuiletea heshima yake miongoni mwa Mataifa.

(e) Kuendelea kuzishinikiza nchi tajiri kutekeleza ahadi yao ya kutenga asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada kwa nchi maskini.

(f) Kuielewa kinagaubaga hali halisi ya uchumi wa kimataifa unaotawaliwa na ushindani wa soko na utandawazi, kuendelea kuukosoa mfumo huu maana unazikandamiza nchi za Kusini na papo hapo kujua namna ya kufaidika na fursa zinazoweza kupatikana kwa maslahi yetu.

(g) Kudai mageuzi katika Umoja wa Mataifa, kwa lengo la kuongeza sauti za nchi zinazoendelea.

(h) Kuitambua jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Tanzanian diaspora*) na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

**Utamaduni na Maendeleo ya Michezo**

118. CCM inaamini kwamba vijana wa Tanzania wana vipaji vya michezo mbali mbali kama walivyonavyo wenzao wa nchi nyingine za Afrika na za Dunia. Kwa lengo la kuendeleza vipaji hivyo na kuendeleza utamaduni na michezo kwa jumla nchini, Serikali za CCM katika kipindi cha 2005-2010 zitaelekezwa kusisitiza yafuatayo:-

**(*Utamaduni*)**

(a) Kuendelea kuenzi na kulinda historia, mila na desturi nzuri za watu wetu na kuzitokomeza mila na desturi mbaya.

(b) Kuhimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya jamii yetu.

(c) Kuweka mipango ya kuwatambua wasanii wa aina mbalimbali pamoja na wasanii wasomi na kuimarisha mipango ya mafunzo ya sanaa hadi Chuo Kikuu.

(d) Kuweka mipango ya kukiimarisha Kiswahili kama kielelezo cha utamaduni wetu.

(***Michezo***)

(e) Kujihusisha kwa nguvu zaidi na maendeleo ya michezo nchini ili kuhakikisha kwamba ushiriki wa Watanzania katika mashindano ya kimataifa unalingana na vipaji vilivyopo nchini.

(f) Kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za michezo na kuwahamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za michezo.

(g) Kukamilisha ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo Dar es Salaam na kwa jumla kuimarisha miundombinu ya michezo nchini kwa lengo la kuinua kiwango cha michezo.

(h) Kuweka mipango ya kuandaa wataalamu katika michezo mbalimbali.

(i) Kuanzisha vyuo vya michezo na kutumia shule na vyuo kama chemchem ya kuwapata wanamichezo bora wa hadhi ya kitaifa na kimataifa. Mashindano ya michezo katika shule na vyuo, ni mambo muhimu sana

(j) Kusaidia viongozi wa michezo mbalimbali kwa mafunzo na ushauri ili kupata uongozi ulio adilifu zaidi na kupunguza migogoro isiyokuwa ya lazima.

(k) Kufufua na kuimarisha michezo ya jadi kama vile mieleka na bao.

(l) Kuweka msisitizo wa michezo kwa wanaume na kwa wanawake pamoja na mpira wa miguu kwa wanawake.

## Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali

### *Watoto*

119. Katika kipindi cha 2005-2010 CCM kupitia Serikali zake inakusudia kuimarisha na kuendeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika zahanati zote katika ngazi za Kata na Vijiji.

(b) Kuendelea kuhakikisha kuwa watoto wanapatiwa kinga za magonjwa katika muda unaofaa.

(c) Kuimarisha utaratibu wa mashirika ya hiari na watu mbalimbali wanaoshughulikia vituo vya kulelea watoto, pamoja na shule za awali.

(d) Kuimarisha na kuboresha viwanja vya kuchezea watoto katika ngazi za Mitaa, Vijiji, na Vitongoji.

(e) Kuendeleza vita dhidi ya dawa za kulevya ili kuwakinga watoto wasiathirike na dawa hizo.

(f) Kuendeleza vita dhidi ya ajira ya watoto.

### *Wanawake*

120. Chama Cha Mapinduzi kinatambua na kuheshimu nafasi ya wanawake katika maendeleo ya nchi, kwa kuweka bayana shabaha za kuendelea kuwaendeleza kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itazielekeza Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kama ilivyokwisha azimiwa na Umoja wa Afrika.

(b) Kuendelea kuwahamasisha wanawake wazitumie fursa za kisiasa katika nyanja mbali mbali, zikiwemo za uchaguzi katika ngazi zote.

(c) Kuongeza nafasi na fursa katika ngazi za uteuzi kwenye utawala, uongozi na menejimenti ndani ya Serikali na taasisi zake.

(d) Kuendelea kupanua na kuongeza nafasi za viti maalumu katika chaguzi za mitaa, vijiji, vitongoji, kamati za shule, kamati za maji, kamati za zahanati, kamati mbalimbali za Bunge na za Taifa, Ubunge na Uwakilishi n.k.

(e) Kuendelea kuwapatia wanawake fursa ya elimu ikiwemo ya uraia ili waendelee kutetea haki zao na kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za jamii.

(f) Kuimarisha mifuko ya mikopo mbalimbali ili waweze kufaidika zaidi.

(g) Kukamilisha taratibu na hatimaye kuunda Benki ya Wanawake.

(h) Kujenga mazingira mazuri ya kuziwezesha benki na asasi nyingine zinazotoa huduma ya mikopo kutoa mikopo kwa masharti nafuu kwa wanawake miongoni mwa wananchi wengine.

***Vijana***

121. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana. Changamoto kubwa ni **kuwaelimisha na kuwashirikisha katika ujenzi wa nchi.**

Kwa kuzingatia malengo hayo, CCM katika kipindi cha 2005-2010 itazihimiza Serikali zake kuwaendeleza vijana kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuendeleza hatua za kuimarisha elimu nchini na kuhakikisha kuwa elimu hiyo inakidhi viwango vya elimu katika karne ya 21.

(b) Kuona kwamba elimu ya kujitegemea, elimu ya ufundi na stadi nyingine inasisitizwa.

(c) Kuona kuwa vijana wanajengeka katika ujasiri, uzalendo na kupenda, kuthamini kazi na kuwa na moyo wa kujitegemea.

(d) Kuwa na mipango ya kuandaa vijana wataalamu katika fani mbalimbali za maendeleo.

(e) Kuendelea kuwahamasisha vijana ili waweze kujiunga katika vikundi mbalimbali vya ushirika ukiwemo ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS).

(f) Kuhamasisha na kuimarisha utoaji wa elimu ya ufundi stadi kwa vijana ili waweze kujiajiri.

(g) Kuimarisha mfuko wa maendeleo ya vijana katika Halmashauri zote, ili uweze kuwanufaisha vijana wengi zaidi kwa usimamizi mzuri na kuwezesha mfuko huo kuwa endelevu.

(h) Kuhamasisha vyombo vya fedha ili vitoe mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana.

(i) Kupanua wigo wa harakati za kiuchumi zinazozalisha ajira nyingi ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

(j) Kuwaandaa vijana kwa ulinzi wa nchi yao, kujenga taifa na uzalendo wa hali ya juu.

***Wazee***

122. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itazielekeza Serikali kuendelea na uimarishaji wa mipango ya utoaji huduma kwa wazee kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuboresha huduma kwa wazee kwenye vituo wanakoishi.

(b) Kuandaa mfumo maalumu wa huduma kwa wazee wasiojiweza kwa kuhakikisha kuwa wanapata huduma za afya ya msingi bila malipo katika vituo vya afya, zahanati, na hospitali zote za Serikali.

(c) Kuendelea kuhakikisha kuwa wazee wanaostaafu katika utumishi wa Serikali na taasisi zake wanalipwa mafao yao bila kusumbuliwa wala kucheleweshwa.

(d) Kuendelea kutumia uzoefu, hekima na busara zao kwa kadiri inavyowezekana;.

***Walemavu***

123. Katika kipindi hiki cha 2005-2010, Chama Cha Mapinduzi kupitia Serikali zake, kitaendelea kuwashirikisha walemavu katika yafuatayo:-

(a) Kupanua na kuimarisha fursa za ajira kwa walemavu.

(b) Kupanua na kuimarisha fursa ya ushiriki wa walemavu katika siasa na uendeshaji uchumi wa nchi.

(c) Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi kama vile elimu, afya, mikopo, na kadhalika.

(d) Kujenga mwamko wa kuzingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu katika ujenzi na utengenezaji wa majengo yanayotumiwa na umma.

***Wafanyakazi***

124. Katika kipindi cha 2005-2010, CCM itaendelea kuwa karibu na wafanyakazi na kuhakikisha kuwa Serikali zinayashughulikia kwa ukamilifu na kwa wakati matatizo yao. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa na Serikali itakuwa pamoja na:-

(a) Kutunga sheria mpya ya fidia kwa wafanyakazi wanaoathirika kazini.

(b) Kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi yote yanayofanywa na Serikali ambayo yanawagusa.

(c) Kujenga mwamko miongoni mwa wafanyakazi na waajiri kuhusu dhana ya mapatano ya pamoja (*collective bargaining*) na kusisitiza matumizi ya dhana hiyo katika kujenga mazingira ya maelewano baina ya wafanyakazi, waajiri na Serikali (**utatu**).

(d) Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu zinazohusu ajira za wageni.

(e) Kuanzisha chombo cha uratibu wa shughuli za hifadhi ya jamii, kutokana na kuwepo kwa mifuko mingi ya hifadhi ya jamii.

(f) Kushirikiana na uongozi uliopo wa wafanyakazi kuandaa mafunzo yanayohusu utetezi wa maslahi ya wafanyakazi katika mfumo wa uchumi wa ushindani wa soko na katika mazingira ya utatu.

**Kuhamia Makao Makuu Dodoma**

125. CCM itaendelea kusisitiza na kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa kuhamishia Dodoma Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha 2005-2010, hatua zifuatazo zitachukuliwa kwa lengo la kuzidisha kasi ya kuhamia Dodoma:-

(a) Kutunga sheria ya kuitambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali na kuweka utaratibu wa Serikali kuhamia huko.

(b) Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa-Dodoma-Arusha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam-Dodoma-Mwanza kama mkakati wa kuendeleza mji wa Dodoma ili uweze kuvutia vitega uchumi.

(c) Kuweka vivutio kwa sekta binafsi ili ishiriki katika uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika ukuaji wa mji, na katika uwekaji wa huduma mbali mbali zinazokidhi mahitaji ya watumishi wa Serikali na wananchi kwa jumla.

(d) Kuongeza kasi ya Wizara za Serikali kuhamia Dodoma, kwa kuwa sasa Serikali inajenga nyumba nyingi za kuishi watumishi.